# SHALOM

. . . ibada, mkutano wa mwaka mpya ukiwa tunauanza tu. Hii ndiyo kampeni yangu halisi ya kwanza tangu mwaka mpya. Lo, nimeshakuwa na siku chache nyumbani, kisha nikashuka kwenda huko Fort Huachuca. Hivyo ndivyo mgepatamka sasa? Siwezi kuona jinsi mnaandika Huachuca mkitumia H. [Nafasi tupu kwenye kanda—Mh.]

2 Hatuta, hatutakuwa na jambo mfano wa kioo cha kutazamia nyuma. Kioo cha kutazamia nyuma huonyesha tu nyuma na kuona pale ulipokuwa. Tunaangalia mbele kuona pale tunapoenda, mwaona. Kile kilicho katika wakati uliopita, Paulo alisema, "Nikiyasahau yaliyo nyuma, nakaza mwendo niifikilie mede ya mwito mkuu katika Kristo." Na hivyo ndivyo tunataka kufanya. Mwanadamu, tunaweza kuangalia nyuma miaka kumi na mitano, kumi na sita iliyopita, nilipokuja Phoenix mara ya kwanza, kumekuwa mambo mengi yaliyotendeka tangu wakati huo, mema na mabaya, ambayo yote huenda Hukumuni, mikononi mwa Mungu. Lakini kile ninachotazamia sasa ni nini nitakachofanya katika mwaka huu ujao kuelekea kuusitawisha ule Ufalme, nikifanya zaidi, yote niwezayo kwa Ufalme wa Mungu.

3 Sasa, adhuhuri hii ninataka kunena Ujumbe huu wa mwaka mpya kwa Kanisa katika Kristo, na ndipo kesho usiku tutawaombea wagonjwa. Na tutatoa kadi za maombi katikati ya . . . Nafikiri ibada huanza saa moja, saa moja na nusu, afadhali mwe hapa thenashara, au saa moja kasorobo, basi, mpate kadi zenu za maombi, ili msitatize sehemu ile nyingine ya ibada.

4 Tunataka kushukuru wale—wale wasimamizi hapa, wa Ramada, kwa kuturuhusu kupata jengo hili kwa mkutano huu, kabla ya mikutano hii. Bwana na awabariki wao.

5 Na sasa ikiwa mnataka kugeukia Maandiko, mahali tutakaposoma, nitasoma kutoka Isaya, sura ya 60, na cha—cha 2, kifungu cha 1 na cha 2. Na Zaburi 62:1-8 Zaburi 62:1-8 kwanza.

*Nafsi yangu yamngoja Mungu peke yake kwa kimya,*
*Wokovu wangu hutoka kwake.*

*Yeye tu ndiye mwamba wangu na wokovu wangu,*
*Ngome yangu, sitatikisika sana.*

*Hata lini mtamshambulia mtu,*

Mtauawa ninyi nyote:

Mtakuwa *kama ukuta unaoinama,*

*Na kama kitalu kilicho tayari kuanguka.*

*Hufanya shauri kumwangusha tu katika cheo chake.*
*Huufurahia uongo.*
*Kwa kinywa chao hubariki,*
*Kwa moyo wao hulaani. Amina.*
*Nafsi yangu, umngoje Mungu peke yake kwa kimya,*
*Tumaini langu hutoka kwake.*
*Yeye tu ndiye mwamba wangu na wokovu wangu:*
*Ngome yangu, sitatikisika sana.*
*Kwa Mungu wokovu wangu,*
*Na utukufu wangu;*
*Mwamba wa nguvu zangu,*
*. . . kimbilio langu ni kwa Mungu.*
*Enyi watu, mtumainini siku zote,*
Mmwagieni *mioyo yenu mbele zake;*
*Mungu ndiye kimbilio letu. Amina.*

6 Napenda jinsi Daudi asemavyo hilo, "ule mwamba." Mnaona, mara nyingi sana, "Mungu ni mwamba wangu." Mnajua kile mwamba unatajwa kuwa Bibliani? *Mwamba* ni "ufunuo."

7 Kama Petro alivyosema, "Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai."

8 Yeye alisema, "Heri wewe Simoni Bar-yona. Na juu ya mwamba huu, ufunuo huu . . ." Mungu alimfunulia. "Mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba yangu aliye mbinguni. Juu ya mwamba huu, ufunuo huu, nitalijenga Kanisa Langu."

9 Na hapa Daudi anapasa sauti, "Mungu ni mwamba wangu, ufunuo wangu!"

10 Sasa katika sura ya 60 ya Isaya, kifungu cha 1 na cha 2.

> *Ondoka, uangaze, kwa kuwa Nuru yako imekufa, Na utukufu wa* B*WANA* *umekuzukia.*
>
> *Maana, tazama, . . . giza litaifunika dunia, Na giza kuu litazifunika kabila zu watu; Bali* B*WANA* *atakuzukia wewe, Na utukufu wake utaonekana juu yako.*

11 Hebu tuombeni. Bwana Yesu, tunapotafakari juu ya Maneno haya, tunaingia sasa katika mwanzo wa ibada hii, kwa heshima Yako. Tubariki, Baba, tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

12 Sasa somo langu adhuhuri hii ni neno moja. *Shalom*. Katika Kiebrania, inamaanisha "amani." Amani, au ni kusalimu, ni "amani iwe kwako," au, "karibu," "habari za asubuhi," aina yoyote ya sa—salamu. Lakini neno muhimu nililopata katika Kiebrania hapa, kuna vitu vingi linavyomaanisha, bali vyote vikihusiana na jambo lile lile, "amani."

13 Tunapokabiliana na huu mwaka mpya, tunakabiliana na vyote viwili, jinsi nimesoma, giza na Nuru. Sasa tunaona kwamba Daudi, akinena hapa, kasema, "Mtumaini Bwana. Weka matumaini yako katika Yeye." Isaya alisema, "Giza kuu litakuja juu ya watu hawa, lakini Kanisa liondoke na kuangaza katika utukufu wa Nuru."

14 Kwa hivyo twaukabili huu mwaka mpya kama tu tunavyofanya miaka yote; kuna ku—kujutia makosa yetu wakati uliopita, na kutazamia siku za usoni za Nuru ya Kristo yenye utukufu. Hapana shaka, tukiishi tukaumalize mwaka huu, tutaona makosa mengi ambayo tumetenda, na tunatarajia hayo tu kwa sababu inaambatana na kufaulu na kutokufaulu. Hiyo ni sheria ya wastani ambayo tunaishi kwayo hapa katika maisha haya. Lakini tuna furahi sana tunaye Mpatanishi ambaye huketi katika mkono wa kulia wa Mungu, kutuombea. Wakati tunapotaka kukubali makosa yetu ambayo tumetenda, basi Yeye huyasamehe. Yeye ni mwingi wa neema na rehema, kutusamehe makosa hayo.

15 Hili giza kuu, nataka kunena juu yake kwanza, kwamba kuna nyingi sana ya hilo ulimwenguni leo, na kunaendelea kuwa kweusi zaidi na zaidi daima. Kila mwaka, tunaona kwamba, kwamba u—ulimwengu unakuwa mweusi zaidi, kunena kiroho, kwa sababu wanapapasa-papasa gizani. Kuna dhambi zaidi. Tukipitia tu kile tulicho nacho, kule kuuawa kwa siri kwa Rais, na kadhalika, na watu wakiwa wanauawa papa hapa nchini mwetu. Ambapo, hatungedhania hayo yangetendeka katika wakati wa ustaarabu wa kisasa, lakini hakika tunayo, kwa sababu giza kuu liko juu ya watu. Sasa, wale ambao hawataigeukia Nuru, basi kuna kitu kimoja pekee ninachoweza kusema kwa ajili ya mwaka ujao, mtazidi kudidimia gizani zaidi na zaidi jinsi mwaka unavyozidi kuendelea.

16 Lakini kwa wale ambao watageuka, katika mwaka huu mpya, kwenye Nuru, basi watang'aa zaidi na zaidi, hadi kwenye ile siku kamilifu ambayo twaitazamia, kufunuliwa Kwake, ambapo giza lote lita—litatoweka. Na sababu hiyo, ndipo nasema, kwa Kanisa la Mungu aliye hai, leo, "Shalom," kwa sababu sisi tu Nuru Zake. Yesu alisema, "Nyinyi ni Nuru ya ulimwengu."

17 Sasa, nabii alisema, "Giza kuu juu ya watu hawa; juu ya watu wa ulimwengu, giza kuu."

18 Mmetambua, katika miaka michache iliyopita, baadhi yenu waume kwa wanawake wa umri wangu, kwamba jinsi kila mwaka, inaonekana kama kwamba giza linaingia zaidi na zaidi? Nilikuwa nikinena hivi majuzi, nikamwambia mke wangu, "Unajua, inaonekana kama kwamba, jinsi miaka inavyoendelea, yaonekana tu kama watu wanaanza kwenda mbali na mbali

zaidi kutoka kwa kitu halisi ambacho wanapaswa kukikaribia zaidi na zaidi."

19 Nimeishaona, miongoni mwa watu. Chunguzeni barabarani na hasa miongoni mwa wanawake. Chunguzeni shauku zao na kile wanachotaka kufanya na wao wana—wao wanabadili nia zao daima. Wanaume wanazidi kuwa kama wanawake, nao wanawake wanazidi kuwa kama wanaume, na inaonekana kama hakuna njia ya kukomesha hilo. Huvuka taifa, nikihubiri dhidi ya jambo hilo, na kurudi tena mwaka unaofuata na linakuwa baya, kuliko lilivyokuwa wakati nilipoanza. Jambo ni kwamba, hao watu wanataka kufanya vyema, lakini, wao, kuna kitu juu yake ambacho hakingewaruhusu wao kutenda yaliyo mema. Kinawagandamiza tu, kikiwalazimisha. Ni—ni kama ukungu mweusi mzito juu ya dunia yote. Sio katika Phoenix peke yake, bali ulimwenguni kote, yaonekana giza limerundikana, likiwa zito na zito zaidi, daima, likiangamiza kabisa utu wa mwanaume na utu uke. Ninazungumza kimaumbile.

20 Na, wao, yaonekana kwamba ile. . . inaingia zaidi na zaidi makanisani. Basi unapoinuka na kusema kitu fulani dhidi yake, ndipo wao wanakulaumu kwa kufanya hilo. Waona, wewe—wewe unaweza kuliona likija, na—na basi unenapo dhidi yake, mtu fulani hukosa kuelewa. Wakati mwingine wanawake hukosa kulielewa, wanaume hukosa kulielewa, wanachukua nia baya.

21 Watu wakati mwingine, watu wema, wamelazimika kustahimili mambo kama hayo ili washikilie haki zao katika vyeo vyao vya kidini, kwa sababu, iwapo hawafanyi hivyo, wanatengwa na ushirika, ndiposa wao huwa—wao wanajitegemea. Na ndiposa mara unapotengwa na watu fulani, basi ni vigumu kushirikiana na mtu mwingine, kwa sababu wakati mmoja walijua ya kwamba ulikuwa mshiriki wa kundi hili lingine, ndipo, "Kulitukia nini *humu*?" Basi yakubidi usimame na kusadiki kwako, au uendelee peke yako, au ukane kusadiki kwako. Kwa hivyo hilo hulifanya kuwa jambo ligumu kweli kweli kwa watu.

22 Na inaonekana kama ni wakati ambapo, huwezi kuona ule msimamo halisi, kama impasavyo mtu kuwa. Mimi. . . Hata nikilirudisha nyuma, kutoka kwa kiroho, sasa mpaka kwa kimaumbile, mimi. . . Ilionekana kwangu kwamba wanaume wanapovaa viatu vya mahameli yenye rangi nyeupe nyekundu, na mambo kama hayo ya kila aina, inaonekana kama tu wamekuwa zaidi kama wanawake. Na wanawake wakivuta sigareti, sasa wamepata sigara, na wao tu. . . na kukata nywele zao kama wanaume; na inaonekana kana kwamba kule—kule kupendeza, utu uke, jambo fulani la kike limeondoka. Na yule mwanamume halisi mwenye utu wa kiume hayupo tena; yale tu aonekanayo akififikiria ni maovu, upande ule mwingine.

23 Nafikiri ni karibu tu kama ilivyokuwa mwanzoni, "kila wazo moyoni mwa mwanadamu laendelea daima kuwa baya." Vipindi vyetu—vyetu vya televisheni na—na redio havikaguliwi. Watu wanaweza kusema chochote, karibu cho chote, watakacho, hata kuapa na kufanya dhihaka chafu, na baya, ambazo—ambazo kwa kweli hazipaswi kuwa, hazinge—hazingeweza kusemwa katika chumba cha kuuzia pombe. Walakini wao waneweza kusema hayo kwenye televisheni na redio, na kuyapeleka moja kwa moja nyumbani mwa watu. Yaonekana kana kwamba giza kuu lafunika jambo lote kwa jumla. Ulimwengu wote waonekana umechafuliwa.

24 Sasa, kwa miaka, nimekuwa nikijaribu kushikilia beramu, Neno la Mungu. Na nimeamua bila shaka mwaka huu ujao kushikilia beramu hiyo kuliko vile nimewahi kuwa maishani mwangu, mwaona, nisimame wima kabisa na hilo Neno. Sasa, natumaini ya kwamba ye yote anayeona niani mwake kuwa ninafanya hivyo ili kuonyesha ni mwerevu, basi, ndugu, dada, bila shaka umekosea. Ninafanya hivyo kwa sababu nimewajibishwa kufanya Hilo. Mimi, nimewajibishwa kudumu na hilo Neno. Chochote lisemacho, usitie tafsiri ya binafsi, liseme tu hivyo. Sasa kuna wengine wanaoweza kulifasiri na kulifanya lisikike tofauti kidogo, bali mimi siwezi kufanya hivyo. Lugha ya pekee niijuayo ni kile kimeandikwa Humu, jinsi tu lilivyo Hivi.

25 Sasa, miaka michache, yapata miaka mitatu iliyopita, ni kama hiyo, ya kwamba, nyumbani, kanisa langu la nyumbani. Roho Mtakatifu alinizungumzia, kasema, "Nenda Tucson, kuna kitu kinachongojea." Nilisimama juu ya jukwaa hili na kumwambia kila mmoja wenu, "BWANA ASEMA HIVI, kuna kitu kiko tayari kutukia." Labda kuna mamia ya watu wanaoketi hapa ambao wanajua hilo. Niliwaambia tu kile nilichoona. Ujumbe ule uko kwenye kanda, *Ni Wakati Gani, Bwana?* Niliona kundi la Malaika, kama pi—piramidi, wakishuka chini kaskazini tu ya Tucson; juu namna *hii*, kaskazini ya Tucson. Na walinizungumzia kitu fulani na sikujua kilikuwa nini. Na siku moja pale. . . Kuna watu wanaoketi papa hapa, wawili wao waliokuwa pamoja nami, nyuma kule wakati hilo lilipotukia.

26 Nao walipiga picha Yake angani. Ilitokea katika—katika gazeti. Nilifikiri nilikuwa na nakala moja. Ninayo. Ndiyo hiyo. Mnaiona hapa katika gazeti liitwalo *Life*, nakala hii, sawasawa tu vile Roho Mtakatifu alivyosema ingekuwa.

27 Na pale walisimama wale Malaika saba kawaida tu kama mnavyoniona mimi nikisimama hapa, na kuniambia nirudi nyumbani mwangu, kwamba siri ambazo wale watengenezaji kote katika nyakati zote walishindwa kuzipata, zile siri za Biblia, ambazo zilishikiliwa na Zile Muhuri Saba, zingefunuliwa. Namhimiza mtu awaye yote, twaa hizo *Muhuri Saba* ukazichunguze upate kosa moja. Mnaona? Kwa sababu zinatolewa kwa uvuvio wa Mungu.

28 Kutangulia hayo, nilihubiri juu ya *Zile Nyakati Saba za Kanisa*, Kisha nikazichora juu ya ubao katika Maskani yangu.

29 Fundisho langu, sihubiri Fundisho huku nje, hamna kitu ila tu kanuni kubwa za kiinjilisti; kwa sababu nipo pamoja na wandugu, huenda wasikubaliane nami, na sitoi Hilo nje mbele za watu hapa. Mimi hujaribu tu kudumu juu ya kanuni halisi za Maandiko, kama zile tunazoamini. Lakini, katika Maskani yangu, wao huyapata kwenye kanda. Ikiwa unaitaka, unaweza kuipata. Ikiwa mchungaji wako hataki uwe Nayo, usiitwae. Waona, hilo ni shauri lako.

30 Lakini mle ndani, nikihubiri juu *Zile Nyakati Saba za Kanisa*, na kuwa na kibali kutoka kwa Mungu; nikizichora, jinsi giza lilivyoingia kanisani, Nikea; na wale malaika wa kanisa, wale wajumbe. Hapana budi ilikuwa kweli kwa sababu, mara tu nilipomalizia kuchora ule wakati wa mwisho wa kanisa Jumapili asubuhi, saa tano; ile Nuru kuu ilishuka ikaingia mle jengoni, mbele ya watu wengi karibu kama wanaoketi hapa; ikashuka na kumemetesha kwenye upande mmoja wa ukuta mbele ya watu hao wote, na kuchora hizo Nyakati za Kanisa sawasawa tu na vile nilikuwa nimeisha zichora pale. Sasa, kuna mamia na mamia ya mashahidi pale kuthibitisha tu hilo.

31 Vema, sasa, tunatambua ya kwamba Mungu daima huonyesha mambo mbinguni kabla hajayaonyesha duniani. Kama vile wale mamajusi walivyoifuata ile nyota, na kadhalika. Ishara ya kimbinguni hutukia, kwanza, ndipo ya kiduniani hushuhudia hiyo ishara ya kimbinguni. Mungu hutenda, hufanya kazi kwa ishara, ishara na maajabu. Zitafuatana na waamini kila mahali. Wayahudi walitazamia ishara daima, kwa sababu walikuwa wateule wa Mungu, na walitazamia ishara. "Tuonyeshe ishara, ndipo tutaamini." Na, basi, wakati wale mamajusi walipokuja na taarifa yao, wale Mamajuzi, ya kuzaliwa kwa Kristo, katika tu mwaka mpya.

32 Sasa tunaona ya kwamba mwezi, katika Biblia, huwakilisha Kanisa. Huonyesha nuru juu ya dunia, jua likiwa halipo. Ufunuo, sura ya 12, kweli hueleza hilo, "mwanamke aliye na mwezi chini ya miguu yake, na jua juu ya kichwa chake." Na jinsi kwamba jua likiwa halipo, jua likisha enda upande ule mwingine, mwezi unaonyesha jua duniani. Kanisa linapaswa kumwonyesha Yesu Kristo kwa walimwengu, katika kutokuwepo kwa Mwana wa Mungu. Sisi sote tunaamini hilo. Ni jambo geni, kama vile limekuwa tofauti.

33 Lakini nikinena hapa, katika 1933, juu ya papa akitua mahali pake kutoka kwa, au akitoka, hasa, Rumi, na kuzizuru zile—zile nchi takatifu. Yeye atakuja hapa pia. Na jambo la ajabu, ni, siku chache kabla hajatoka Rumi, kwa mara ya kwanza kwa hili kuwa katika historia, mwezi ulishuka na ukapatwa kabisa. Hilo tu, ilikuwa nini? Ukitia kivuli kabisa

Nuru iliyorudishwa ya Jua. Katika hili, alinena na baba wa Kiothodoksi; na wote wana mapatano, "Papa anatenda hili kwa ajili ya ushirika, ushirika wa ujirani mwema." Ambao husikika, kwa sikio la kawaida, jambo la ajabu sana ambalo lingelitukia. Bali kwa sikio la kiroho, ni giza. Na jinsi sisi makanisa, sisi Wapresbiteri, Wamethodosti, Wabatisti, na Wapentekoste, tungeweza kuungana na uchafu wa namna hiyo na huku twajua Biblia yetu hutufundisha tofauti! Ni jambo la kustaajabisha kwangu mimi, jinsi mtu aliyejawa na Roho anaweza kuketi mahali na kusema, "Inaonekana kiroho kuwa mahali pa namna hiyo." Kwangu mimi, ni chukizo kubwa mno.

34 Sasa, mimi nadhani ninyi mna hilo hapa Phoenix. Ikiwa ye yote. . . Ni wangapi walio hapa wameisha kuona nilipozichora picha za Nyakati za Kanisa? Inueni mikono yenu. Nadhani. . . Mnaona jinsi Bwana alivyozichora angani, juzi usiku? Sawa sawa tu na zilivyochorwa kule Maskanini. Kikamilifu sawasawa na vile Roho Mtakatifu alivyozitoa kwa uvuvio, miaka mitatu iliyopita, hapo Maskanini, na pale ikatokea angani. "Kwa vinywa vya mashahidi wawili au watatu, hebu kila neno lithibitike." Roho Mtakatifu kwanza alienenda kwa upako; nikazichora jukwaani. Kisha Yeye akashuka Mwenyewe na kufanya dhihirisho Lake, kama mwezi na Nuru zikitiwa giza, zikitiwa giza, na Wakati huu wa Laondikia ukitokomea katika giza tupu tena. Na hapa yuashuka chini na kudhihirisha hilo juu ya mwezi, mara tu wakati ambapo makanisa yote yanaungana katika umoja wa muungano wa makanisa.

35 Si ajabu, kama Isaya alivyosema, "Giza kuu limo juu ya dunia, juu ya watu hawa."

36 Ninajua ni jambo lisilopendwa na watu kunena dhidi ya dhehebu, bali hiyo ndiyo alama ya mnyama. Hilo ndilo jambo linalotuchukua moja kwa moja hata kwake. Linafanya sanamu kwa yule mnyama. Mimi sisemi hilo nipate kushikwa na hasira. Mimi nasema hilo kwa sababu ni Ukweli ndugu zangu.Siku itakuja ambapo Phoenix utainuka, na labda nimekwisha ondoka, bali mtajua ya kwamba hilo lilikuwa BWANA ASEMA HIVI. Ni kweli. Na jinsi huyo Roho Mtakatifu mkuu ameisha thibitisha zile Jumbe na kutabiri yale mambo bila kukosea hata mara moja! Na mbona sisi hupapasa gizani? Mbona watu wasiamke kabla haijachelewa sana? Mojawapo ya siku hizi, mtakuwa mmechelewa sana, wakati mmeishapata ile alama, ndiposa hapatakuwa. . . Hamna kitu kinginecho mwezacho kufanya juu yake wakati huo, mtakutwa katika utaratibu huo, huku mmetiwa alama pamoja na huo utaratibu.

37 Mbona hamji kwake Kristo, mjazwe na Nuru ya Injili ya Yesu Kristo, Nguvu Zake za ufufuo zinazoweza kuwaweka huru na kuwafanya mshumaa unaowekwa juu ya mlima? Haidhuru kunakuwa giza jinsi gani. Mwasema, "Vema, kwa nini tufanye hilo? Wengine wote. . . " Sikilizeni, sasa hivi ndio wakati wa

kuiachilia iangaze, wakati kuna giza zaidi. Huo ndio wakati Nuru huangaza vema zaidi, ni wakati uko gizani. Yatubidi daima kuachilia Nuru iangaze palipo na giza.

38 Nabii akisema, "Giza kuu litakuwa juu ya watu hawa," na bila shaka ni Kweli.

39 Sasa tunatambua kilichoufanya mwezi kurudisha ile nuru. Mungu akionyesha, kwanza, juu ya ubao wa kuandikia; pili, kwa Uwepo Wake Mwenyewe; ndipo akaonyesha ishara mbinguni. Na ndipo kutoka Rumi akaondoka papa, kuelekea Palestina; ambayo, kwa jicho la kawaida, watu walipaza sauti na kuanguka kifudifudi, na kumwabudu huyo mtu. Simpingi zaidi ya vile ningempinga muhudumu ambaye angaliungana na mambo kama hayo. Yote ni roho yule yule.

40 Inaonekana kama kwamba giza kuu limetulia juu ya watu hata wanafikiri jambo la pekee lilipo la kufanya ni kuenda kanisani na kuwa mtu mwema sana, kuandika jina lako katika kitabu, na jambo dogo la siri, "Mungu ataupindua ufunguo utakapokufa, na kuigeuza hiyo roho iliyo ndani yako, Kwake." Umekosea. Unapokufa, roho hiyo iliyo ndani yako, hivyo ndivyo utakavyokuwa milele. Na kumbukeni, wale Mafarisayo, Masadukayo, na kadhalika, walikuwa watu wa dini sana.

41 Mungu ni Mungu mwenye wivu. Yeye ni mwenye wivu, naye humtaka mke Wake awe msafi. Yeye humtaka awe bikira, safi. Hana chochote cha ulimwengu ndani yake, hata kidogo; ni Neno Lake kwa jumla, sehemu Yake. Ni lazima tuwe sehemu ya Neno. Sio sehemu ya kanuni za imani; sehemu ya Neno! Sio sehemu ya kanisa; sehemu ya Bibi-arusi! Kanisa limehukumiwa, tunajua ya kwamba linaelekea kwenye giza la nje, bali Bibi-arusi anaelekea juu.

42 Sasa laiti watu wangeamka kwa muda mfupi na kutambua jambo hilo kuu ni nini. Ni kiburi ambacho hutenda hayo. Ni watu ambao—ambao hutaka kuenenda kama walimwengu wengine. Huwezi kufanya hivyo. Wewe si wa ulimwengu. Unafikiri mwanamke anayelala katika jeneza atataka ajue kwamba ameisha pakwa rangi nywele zake, au chochote kile unachotaka kukiita? Unafikiri angejali jinsi alivyovalia kama analala katika jeneza, au mwanaume fulani? Hawangefanya hivyo.

43 Na hiyo ndiyo sababu, leo, kuna mambo mengi sana ambayo hatuna budi kuyaigiza toka kwa jirani zetu, au mcheza sinema fulani wa kihollywood, au mtindo fulani, au kitu cha namna hiyo, ni kwa sababu bado hatujamfia Kristo na Neno Lake. Kuna nini makanisani? Tumo gizani, tukipapasapapasa gizani. Kasema, "Kungekuwa na giza kuu juu ya watu." Giza kuu juu ya watu sasa!

44 Hii yote inamaanisha nini? Inamaanisha hili, kwamba wakati ulimwengu . . . kilichofanya mwezi kufifia, ni kwa sababu lile—lile jua . . . dunia iliingia kwenye kivuli cha jua, lililokuwa

likirudisha mng'ao wake juu ya dunia. Ulimwengu uliingia kivulini. Hiyo ndiyo shida ya kanisa. Hiyo ndiyo shida ya Wapresbeteria, Wamethodisti, Wapentekoste. Hiyo ndiyo shida kwetu sote. Ulimwengu huzuia kabisa Nuru ile tunayopaswa kuwa tunarudisha, unajizungusha wenyewe na kuingia ndani Yake, na, zinapopitana, hutupa giza juu yake.

45 Na ulimwengu umeishaingia kanisani, katika—katika jina la dhehebu, katika jina la kanuni fulani za imani, na "sisi tu wenye dini na *hili* lote na *hili* lote," bali bado hukataa nguvu za kufufua za Kristo zithibitishe Neno Lake ambalo limetabiriwa kwa ajili ya siku hii. Kunaweza tu kuwa na Nuru kupitia kwa Neno la Mungu. Tunajua hilo. Mungu, hapo mwanzo, kasema, "Iwe nuru," na ikawa nuru, thibitisho la Neno Lake ambalo alikuwa aishanena.

46 Weusi, kukawa giza! Ulimwengu ulilengana na kurudishwa kwa nuru ya jua mwezini, na ukatia giza. Hivyo ndivyo hasa ilivyotendeka katika ya kimaumbile ama katika ya kiroho. Kama ilivyotendeka katika ya kimaumbile, ilionyesha kimbele na kutuambia sisi, hicho ndicho hasa kilichotukia.

47 Sasa, mnaona jinsi hilo hutokea mwishoni. Wengi wenu enyi vijana, haitawapasa kuzeeka sana mpaka mtakapoliona, kwa vyovyote, endapo mtaishi miaka mitatu au minne zaidi.

48 Mwezi sasa, tuko katika Wakati wa Kanisa la Laondekia. Katika Wakati wa Kanisa la Laondekia, katika makanisa yale mengine yote, la Laondekia, la mwisho, ni wakati wa kanisa lenye uvuguvugu, Kristo alikuwa nje ya hilo Kanisa. Msomaji ye yote wa Biblia anajua hilo. Ufunuo 3, Yeye alikuwa nje ya hilo kanisa, akijaribu kupata njia ya kurudi ndani tena, na haisemekani kamwe Yeye aliingia ndani. "Lakini wote Yeye aliowapenda, Yeye aliwakemea na kuwarudi." Ujumbe ungewakemea na kuwarudi wale ambao Yeye aliwapenda. Sasa, alikuwa anabisha, akijaribu kuingia ndani: giza liliizuia kabisa, ndivyo imetendeka hasa. Nuru ile imekuwa ikiangaza, hivi karibuni yote itafunikwa kabisa. Yote itaingia katika kuundia sanamu yule mnyama. Na tunajua kile hilo lamaanisha, basi huo ndio wakati wa mwisho.

49 Mungu, hapo Mwanzo, alitenganisha nuru na giza, na hilo ndilo Mungu anafanya tena. Mungu hutenganisha nuru na giza. "Hapo mwanzo," Yeye alisema, "iwe nuru." Sasa, kumbukeni, haiwezekani kuwepo nuru nje ya Neno la Mungu. Jua lile lililoko kule nje ni Neno la Mungu, likithibitishwa. Kulikuwa na giza kuu juu ya nchi, ukungu na umande juu ya nchi, na Mungu akasema, "Iwe nuru." Sasa vipi kama nuru haikutokea? Basi haingelifaa kitu Kwake kunena. Bali Yeye aliposema, "Iwe nuru," na nuru ikajitokeza, ikithibitisha ya kwamba Neno Lake lilikuwa sahihi. Tunaishi kwa nuru hiyo leo.

50 Na Nuru ya pekee ambayo tunaweza kuwa nayo leo, kanisani, ni Mungu akithibitisha Nuru Yake kwa kizazi hiki.

51 Kila kizazi kiligawiwa kiasi fulani, kilichotendeka katika siku zao. Sote tunajua hilo. Manabii walijitokeza. Wao, Neno la Bwana liliwajilia, walilifahamu. *Mwonaji* katika Agano la Kale, humaanisha hivyo, "mtu ambaye Neno limefunuliwa kwake." Na jinsi wanavyolijua, ni kwa sababu hujua kimbele mambo ambayo yatatokea. Ndiposa Neno la Bwana liliwajilia wao, kila wakati.

52 Yesu alisema kwa Yohana, juu ya Yohana, "Yeye alikuwa taa iwakayo na kung'aa, kwa muda." Kwa nini? Isaya, miaka mia moja na kumi na mbili kabla yeye kuzaliwa, alisema, "Kuna sauti ya mtu aliaye nyikani." Malaki sura ya 3, ilisema, "Angalieni, namtuma mjumbe Wangu, mbele Yangu, kuitengeneza njia mbele Yangu." Mnaona, Yeye alikuwa Neno lile likithibitishwa. Neno lililoahidiwa kwa siku hiyo, Yeye alikuwa ile nuru, kwa sababu alikuwa akilifanya litimie Neno lile lile ambalo Mungu alikuwa amelinena juu yake.

53 Na alipokuja Yesu, Yohana alisema, "Sina budi kufifia sasa; Yeye hana budi kutokea dhahiri." Naye alikuwa ile nuru.Kote katika zile nyakati jinsi Mungu alivyonena juu ya kuja kwa saa ile, kupitia nyakati zote!

54 Hao makasisi walikosaje kuiona? Walishindwaje? Hao Mafarisayo na Masadukayo walikosaje kuiona? Yeye alisema, "Mwayachunguza Maandiko, kwa sababu mnadhani kwamba ninyi mna Uzima wa Milele ndani Yake, na Hayo Ndiyo yanishuhudiayo Mimi." Walikosaje kuiona, ndugu zanguni? Ni kwa sababu ilikuwa imeisha tabiriwa kwamba wangefanya hivyo.

55 Na hivyo ndivyo ilivyo leo, ya kwamba giza kuu linawajilia watu, na tuko hivyo! Mungu amegawa Neno Lake lidhihirishwe siku hii, na ndilo Nuru ya pekee tuliyo nayo, na Mungu atamruhusu mtu fulani alidhihirishe Neno hilo. Mtu fulani atafanya hivyo. Yeye aliliahidi, na Yeye hufanya kazi tu sawasawa na vile Yeye daima alifanya kwalo.

56 Yeye hajawahi kamwe kubadili mtindo Wake wa kazi. Yeye hutabiri kile kitakachotukia, kisha Yeye hutuma mtu fulani na kuthibitisha hilo. Nalo hupitia juu ya vichwa vya mamilioni, kwa sababu, giza hufunika dunia wakati huo. Nao watu hupenda giza zaidi ya vile wao hupenda Nuru, kwa sababu giza lina anasa nyingi.

57 Nimeisha ona mchezo wa Hollywood, si muda mrefu uliopita, kasema, "Maisha huanza baada ya machweo." Huo ndio wakati mauti huanza; vilabuni hivi vyote vya usiku, na ambapo wao wanadhani wanaishi. Wao wanakufa.

58 Hapo mwanzo, Mungu alitenganisha nuru na giza. Yeye amefanya hivyo daima. Yeye hufanya nini? Yeye husukumia hilo,

kwa kuja kwa nuru, Yeye husukumia giza hata upande wa pili wa dunia.

59 Na hilo ndilo hasa linaloenda kutendeka sasa. Ni kabla tu ya mchana. Ile nyota ya asubuhi imeisha tokea kuusalimu mchana unaokuja. Na Roho Mtakatifu anaonyesha Nuru Yake. Wakati waja ambapo Nuru na giza hazina budi kutenganishwa, moja kutoka kwa nyingine. Kanisa na kanuni zake litatwaa taratibu za siku; na Kristo na ahadi Yake ya Nuru-Neno watanyakuliwa. Hilo ndilo jambo pekee ambalo lililosalia kufanywa nao. Ni siku, leo, ni kupambazuka kwa siku mpya, kwa wengi ambao wanatazamia Kuja Kwake.

60 Watu wengi mno, wema na wenye mioyo minyofu leo, hilo ndilo linalowasha mioyo yao, watu wengi sana, wema na wenye mioyo misafi kama Mariamu na Yusufu. Walikuwa wanatoka kwenye karamu, nao wakampoteza Yesu. Watu wengi hufanya jambo lilo hilo leo, wakidhania ya kwamba Yeye yu pamoja nao. Sasa, nataka kuweka nuru hii dogo kwenu, kuwaonyesheni jinsi Neno la Mungu lisivyokosea.

61 Sisi sate hapa, alasiri hii, tulio Wakristo, tunaamini ya kwamba Yesu Kristo alikuwa Neno la Mungu, lililodhihirishwa. Tunaamini Yeye alizaliwa na bikira. Yeye alikuwa maskani ambamo Mungu Mwenyezi alikaa hapa duniani. Sio nabii tu, sio mtu wa kawaida tu, bali Mungu Mwenyewe akidhihirishwa katika umbo la mwanadamu. Yeye alikuwa *Imanueli*, "Mungu pamoja nasi." Tunaamini hivyo, kwa mioyo yetu yote. Na sasa tazama wakati Maritha au. . .

62 Mariamu, hasa, na Yusufu, wakidhania Yesu alikuwa pamoja nao, walikuwa wakiona tu Yeye alikuwa pamoja nao, wakidhania, "Haina budi kuwa ni vyema tu. Inampasa Yeye kuwa pamoja nasi." Lakini walikuwa wamekosea vibaya. Yeye hakuwapo.

63 Watu wengi, wema, wako hivyo, leo. Wanawaza, wanaiona saa ikikaribia, wanajua kuna kitu fulani kinajitayarisha kutendeka, wanafanya nini? Wao huenda kujiunga na kanisa, wakidhania Yeye yu pamoja nao. Wanasalimiana kwa mkono na kuhubiri, wakidhani hayo ndiyo yote wanayopaswa kufanya, "Yeye yu pamoja nao." Walipewa kipa imara au walibatizwa kwa njia fulani, hayo ndiyo yote wanapaswa kufanya, wakidhania Yesu yu pamoja nao. Ndugu, dada, kama tu Mariamu, Yusufu, wa kale, watu wenye moyo safi kweli kweli, hata hivyo wamekosea.

64 Maisha yako huthibitisha kama Yesu yu pamoja nawe au la. Maisha yako huonyesha kama Yeye anakaa *hapa*, au kama Yesu yungali katika mbingu Zake au la, chochote ulicho. "Kazi nizifanyazo Mimi, wewe nawe utazifanya." Ungewezaje uwe na Kristo ndani yako, kisha Roho yule yule aliye ndani yako akane Neno Lake, na badala yake unatwaa kanuni za imani? Hawezi

kufanya hivyo. Yeye angalijishinda Mwenyewe kwa kulikana Neno Lake Mwenyewe.

65 Kwa sababu tu mtu fulani aliweka tafsiri baya Kwake? Una Biblia, unaweza kusoma kama mtu mwingine awaye yote. Uwe na unyofu wa moyo.

66 Daudi alisema, "Mweke Yeye daima mbele ya uso wako." Jueni ya kwamba tunapokabiliana na mwaka huu mpya, tunaukabili katika nguvu za ufufuo wa Kristo. "Yeye yuko mbele yangu daima. Sitatikisika."

67 Tazameni jinsi Neno lisivyokosea. Mariamu na Yusufu... Sasa kwenu, enyi marafiki zangu Wakatoliki wapendwa, mliosema Mariamu alikuwa mama wa Mungu. Mariamu hakuwa hata mama wa Yesu, sebuse mama wa Mungu. Angewezaje kuwa? Sawa. Hata mara moja Yeye hajamzungumzia kamwe kama mamaye; hata kidogo.

68 Walimjia Yeye wakati mmoja, na kasema, "Mama yako na ndugu zako wanakungoja nje."

69 Alitazama kusanyiko lake, kasema, "Mama yangu ni nani? Ndugu Zangu ni nani?" Alitazama wanafunzi Wake, kasema, "Wale watendao mapenzi ya baba Yangu, hao ndio walio mama Zangu..."

70 Juu ya msalaba, alipokuwa akifa, pia alinena jambo lilo hilo. Yeye alimwambia Yohana, Yohana hapa, mtu huyu, "Mwanangu, mtazame mamako!" Si "Mama, mtazame mwanao." "Mwanamke, mtazame mwanao!" Sivyo, mwaona, yeye hakuwa mama wa Mungu kamwe.

71 Alikuwa tu tumbo la uzazi la kuazima ambalo Mungu alitumia; si zaidi ya mwanamke mwingine ye yote ambaye Mungu anawaza kufikiria kumtumia. Yeye angaliweza kutumia tumbo lako la uzazi la moyo wako, kumtangaza Mwanawe, ikiwa wewe—ikiwa wewe ungalimwachilia Yeye kufanya hivyo. Mnaona? Si mama wa Mungu. Pangalikuwa na msisimko, hata kuwa mbegu ya Mariamu. Yeye hata hakuwa mbegu kutoka kwa Mariamu.

72 Jambo lote kwa jumla lilikuwa Mungu, muumbaji. Ikiwa Adamu wa kwanza kule nyuma aliumbwa bila baba na mama, Adamu wa pili alikuwa jambo lile lile. Na jambo lolote dogo kuliko hilo halingemfanya Yeye kuwa sawa Naye. Hiyo ni kweli. Mungu yule yule aliumba mwili ambao Yeye Mwenyewe alikaa ndani yake.

73 Sasa tunatambua, angalia jinsi, angalia, ikiwa Mariamu alikuwa mama wa Mungu, jinsi alivyoteleza, kule. Alisema, "Baba yako nami tumekutafuta Wewe kwa machozi." Akikana uzazi wa kibikira, "Baba Yako, Yusufu, nami, tumekutafuta Wewe."

74 Mwangalie yule Mvulana mwenye umri wa miaka kumi na miwili, Mtoto wa miaka kumi na miwili, akisema, "Hamjui ya kuwa imenipasa kuwa katika kazi ya Baba yangu, nikijadiliana na madhehebu kule?" Sasa, ikiwa Yeye alikuwa katika kazi ya Yusufu, Yeye angalikuwa huko chini kwenye duka la seremala. Yusufu hakuwa baba Yake. Mungu Ndiye alikuwa Baba Yake. "Hamjui yanipasa kuwa katika kazi ya Baba Yangu?" Huko juu, mwenye umri wa miaka kumi na miwili, pamoja na hao makuhani walioelimika. Hajakuwa hata siku moja shuleni, hata hivyo walistaajabishwa na hiyo hekima. Basi tazama katika . . .

75 Yeye alikuwa Neno. Yeye alipozaliwa, alikuwa Neno. Yeye yungali Neno. Angalieni, Neno halitatwaa muigizo. Alisema, "Baba yako nami tumekutafuta Wewe kwa machozi."

76 Kasema, "Hamjui ya kwamba imenipasa kuwa katika kazi ya Baba Yangu?"

77 Alimkemea mama Yake Mwenyewe? Kwa nini? Yeye alikuwa Neno. Pangekuwa na swali niani mwa mtu fulani, ikiwa Mariamu hapa, ambaye siku moja alisema "Roho Mtakatifu" alimtilia uvuli na akamzaa Mtoto Mwanamume, kisha hapa anamwita Yusufu babaye. Neno halikosei. Haliwezi kushindwa.

78 "Hamjui ya kwamba yanipasa kuwa katika kazi ya Baba Yangu?" Basi Yeye alikuwa katika kazi ya Baba, si—si kazi ya Yusufu, kutengeneza milango na—na vitu vya seremala. Yeye alikuwa katika kazi ya Baba Yake, akizinyosha siasa za kidini walizokuwa nazo siku hiyo. "Hamjui ya kwamba yanipasa kuwa katika kazi ya Baba Yangu?" Naam, bwana.

79 Watu wengi leo, waliomo katika mengi ya makanisa haya mazuri, wanaingia katika hilo baraza la kanisa; si "wanaingia" ndani, tayari wako mle. Wanatambua ya kwamba hilo ndilo tu jambo la kufanya, "Kwa urafiki, uzuri, kwa nini sisi sote tusiungane?" Kwa nini, wamekuwa wakijaribu, wote kwa miaka, kuwafanya Wamethodisti wote Wabatisti, na Wabatisti wote Wapresibateria; Wapentekoste wamejaribu kuwafanya wale wengine wote Wapentekoste. Hamwezi kufanya hivyo, lakini baraza ndilo jibu kwenu. Hilo ndilo jibu, kile Biblia husema wao watatenda, na hicho ndicho tu kile wameisha tenda hasa. Makanisa ya kirafiki ni, naam, bwana, muungano, "Sawa, hebu tuwe na ushirika!"

80 Biblia ilisema, "Wanawezaje watu wawili kutembea pamoja wasipokuwa wamepatana?"

81 Baadhi yao hukana kuzaliwa na bikira. Asilimia themanini ya makanisa ya Kiprotestanti hukana kuzaliwa na bikira. Nao hukana ubatizo wa Roho Mtakatifu. Wao hukana ishara za Kuja Kwake, zile Nguvu za ufufuo. Wao hukana Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Mnawezaje, wakati Mungu aliweka machafuko haya yote ulimwenguni kwa sababu mwanamke siku moja alishuku sehemu moja dogo ya Neno Lake? Shetani

alimwambia huyo Kweli, yote ila jambo moja, bali hilo lilikuwa ndilo jambo lililosababisha shinda yote. Sasa, ikiwa huzuni hizi zote kubwa na majonzi ambayo inakubidi kuyashughulikia, kwa sababu sehemu moja dogo Yake ilitiliwa shaka, unafikiri sehemu moja dogo ya shaka itatuingiza ndani?

82 Hiyo ndiyo sababu Yesu anakuja kwa Bikira safi, mtakatifu, aliyejazwa Roho Mtakatifu, na asiye wa ulimwengu, bali wa Nguvu za Mungu. Lo, ni ajabu jinsi gani kujua kuna uwezekano wa kuingia katika Kundi hili! Unaingiaje? Hautafanya hilo kamwe kwa kujiunga na dhehebu. Utafanya hilo utakapobatizwa kwa Roho Mtakatifu, katika Mwili wa siri wa Yesu Kristo, ukainuliwa pamoja Naye katika ufufuo, huru na mauti na dhambi. Hiyo ndiyo njia ya pekee.

83 Giza! Madhehebu makuu, na kundi kuu la watu wanaungana na kupanga mawazo yao juu Yake, na hilo huwatupa ninyi moja kwa moja nyuma kwenye msukosuko kama ilivyokuwa mwanzoni. Hakuna matumaini hata kidogo katika jambo hilo; mumekwisha tu. Na wao wote huonekana kuwa wameamshwa sana kuhusu makanisa haya yaliyo rafiki, walidhani kwamba Mungu atakuwa nao. "Vema, ule Utawala wa Miaka Elfu utaanza wakati baraza lote litakapokusanyika juu pale, na mienendo yote ya ekumenia, na kadhalika," nao waungane. Wanafanya nini? Wanamfanyia sanamu yule mnyama, nguvu, ambapo wote wasio wa madhehebu, na kadhalika, ambao hawataungana nao, watazuiwa kabisa. Tazama tu na uone kama hilo litatendeka.

84 Ninalo limeandikwa hapa chini, siku ile ile sisi. . .Bwana aliniruhusu kuona hayo katika mwaka wa 1933. Na hapa liko sawasawa tu na vile yeye. . .vile lilivyosema, likija tu vile vile, jinsi papa angeondoka Rumi, na kadhalika.

85 Sasa, wao ni watu wema, bali wamekosea. Yusufu na Mariamu walikuwa watu wazuri, bali waliokosea kweli kweli. Lakini ilikuwa nini? Mungu alimtumia Mvulana wa umri wa miaka kumi na miwili kuonyesha kuwa Neno hilo lapaswa lidumu safi, jinsi lilivyokuwa hasa, kile lilichosema mara ya kwanza, "Yeye alizaliwa na bikira," na hicho ndicho Yeye alichokuwa.

86 Wakidhania Yeye alikuwa pamoja nao walipojiunga na makanisa, na kadhalika, lakini sivyo. Sasa, lakini kwa Wateule. . .sasa, hilo ni giza, na ningalidumu juu ya hilo kwa saa nyingine.

87 Lakini kwa Wateule, watu wa Thamani na Walioitwa, Watakatifu wa Mungu, Mimi nasema kwenu, mwaka huu unaokuja: Shalom, amani ya Mungu!

88 Saa imefika! Kama ningalikuwa kule nyuma kabla ya siku ambazo ulimwengu uliumbwa, na nikatazama chini na kuona jambo lote kwa jumla, na Baba aniambie mimi, "Ni siku gani

wewe ungalitaka kuishi?" Ningalisema sasa, sasa hivi! Hii ndiyo saa! Hii ndiyo saa kuu zaidi ambayo Kanisa limewahi kuingia kwake, kabla tu ya kuja kwa Bwana-arusi. Lo, Kanisa halisi la Mungu aliye hai lapaswa kuwa moto, likiwaka, na Nuru ya Injili ikithibitishwa kati yao. "Ondoka uangaze, kwa kuwa Nuru imekujia wewe," Nuru ya siku hii. Isaya alikuwa nuru ya siku yake. Nuhu alikuwa nuru ya siku yake. Kwa nini? Alikuwa na Neno lililodhihirika. Na Injili, Maneno ya Biblia kwa siku hii, ndiyo Nuru ya siku. Ni wakati mtukufu namna gani tunaoishi!

89 Sasa, "habari za asubuhi" humaanisha *amani*. Giza linakusanyika. Linakusanyika kwa nini? Kuonyesha Nuru. Isaya 60:1, "Ondoka ukaangaze, kwa kuwa nuru imekujia wewe." Hiyo ndiyo sababu ninaweza kusema, "Shalom," Nuru imeisha kukujia wewe, amani ya Mungu kwa Mwanamke mteule, kwa Bibi mteule; wale ambao Mungu, kabla ya misingi ya ulimwengu, aliwaita watoke na kuwaagizia Hilo.

90 Wale wengine wao hawataiona kamwe. Hawatajua kamwe neno lolote juu Yake. Biblia ilisema hivyo. Na Yesu alisema, "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba Yangu kwanza; na wote alionipa Baba watakuja." Hiyo ni . . .

91 Pale alisimama Yuda, Nuru ikiangaza *hapa* juu, lakini nyuma moyoni mwake mlikuwa mbegu nyeusi. Shindano la kuamua lilipofika, giza ikajionyesha.

92 Hapa alikuwepo masikini mwanamke mzee, ametiwa giza kote, juu *hapa* mbele, bali *humu* chini alikuwa mbegu iliyochaguliwa tangu awali. Na Nuru ilipokuja, ikaitawanya giza, na ikaionyesha. "Tunajua Masihi yuaja, na, Yeye ajapo, Yeye atatuonyesha mambo haya."

Yesu alisema, "Mimi Ndiye."

93 Lakini Yuda aliishuku, ingawa alidhaniwa kuwa anatembea Nuruni. Mnaona, Nuru *hapa* juu haijalishi; ni Nuru iliyomo *humu* ndani ambayo ina maana. Nuru iliyo juu *hapa* itatembea na kushirikiana, na kitu chochote kile; bali hapo nguvu halisi za Mungu zijapo ndani, haziwezi kurudia mbegu *hii* ambayo imekufa, itajionyesha katika dhehebu.

94 Lakini irudipo *hapa* ndani, mbegu halisi, iliyochaguliwa tangu awali, hapo Nuru hiyo iingiapo humu ndani, huonyesha giza yote mbali nawe, na hukuingiza katika ushirika pamoja na Kristo. Yeye Ndiye ambaye alikupa wewe Uzima kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, kama sivyo hutakiona kamwe, kile alichosema Mungu.

95 Sasa, kwenu Mbegu iliyochaguliwa tangu awali, Shalom! Amina. Amani ya Mungu na idumu juu yenu, kwa sababu tuko karibu mwisho sasa. Tuko karibu sana mwisho. Tutazungumza juu ya kundi hilo, kwa muda mfupi. Shalom!

96 Nuru ya Mungu imeisha kuja. Lile Neno, Nuru, linathibitishwa tena, ili kwamba mkaweze kuona madhihirisho ya ahadi ya Mungu kwa ajili ya siku hii. "Mwayachunguza Maandiko, ndani Yake mnadhani mna Uzima wa Milele." Yanashuhudia siku ambamo tunaishi. Nuru ya siku ni nini? Biblia iliahidi nini kwa ajili ya siku hii? Mnaona ni saa ipi!

97 Si ajabu Yesu aliwakaripia kwa kutokumwamini Yohana. Yeye alikuwa nuru, kwa sababu nabii alisema angekuja. Na alikuwa pale, nuru iliyodhihirishwa. Hawakuiona. Hawakuifahamu; walidhani alikuwa Masihi, *nao* wakafikiria jambo lingine, na *hili* lingine. Walishindwa kuiona.

Yesu akatokea. Nuru mbili haziwezi kuangaza wakati mmoja.

98 Hakuwezi kuwa nuru ya kanisa na Nuru ya Mungu zikiwaka wakati mmoja. Haina budi kuwa ni Nuru ya Mungu ikizima nuru ya kanisa. Na hilo ndilo hasa linalotendeka leo. Mungu anatenganisha ukanisa na Nuru Yake ya Neno lililoahidiwa kwa ajili ya saa hii tunamoishi. Hiyo ni Kweli, rafiki. Huenda ikawa hutaki kuamini hilo, bali ngojea tu uone kama ndiyo ama sivyo. Usingojee, ni afadhali uingie sasa hivi panapo nafasi ya kuingia ndani.

99 Neno ni Nuru linapothibitishwa. Mpaka Neno, lililoahidiwa kwa ajili ya siku hiyo, limethibitishwa, basi si Nuru. Haliwezi kuwa. Kama Mungu alisema, "Iwe nuru," na pasitokee jua, hamna ishara ya nuru. Lakini Mungu aliposema, "Iwe nuru," ikawa nuru. Mungu alipoahidi Masihi, Masihi alikuja, basi Neno Lake lilitimia na Yeye alikuwa Nuru ya wakati ule. Wakati Yeye alipomwahidi Nuhu na kuahidi hao wengine, na kuendelea, wao walikuwa nuru ya wakati ule.

100 Na kuna Nuru ya wakati leo, hiyo ni Yesu Kristo katika nguvu za ufufuo Wake, Neno Lake ambalo limeahidiwa kwa ajili ya siku hii. "Kazi nizifanyazo Mimi, mtazifanya pia; na kubwa kupita hizi mtazifanya, kwa kuwa Mimi naenda kwa Baba." Kazi kubwa, mambo makubwa kuliko aliyotenda? Mnaliamini? [Kusanyiko, "Amina."—Mh.] Mimi naliamini. Inaonekana nyenyekevu. Inaonekana kama inapitia juu ya vichwa vya watu. Tazameni Yeye alipokuwa hapa duniani, mgezifanyaje kazi "kubwa?" Nimeisha fasiri hilo, mara nyingi, "zaidi," bali jambo lile lile. "Kubwa," Yeye alisema katika Yohana Mt. 14:12, "kazi kubwa kuliko hizi mtazifanya."

101 Je, mlitambua? Yeye alipokwenda kuyafanya maji kuwa divai, Yeye alitwaa maji, kwanza; kitu ambacho tayari kimeumbwa, na kukigeuza kuwa divai. Yeye alipolisha watu elfu tano, Yeye alitwaa samaki ambaye zamani aliogelea majini, akammega, kamtoa, na kuzidisha kiumbe. Yeye alitwaa mkate ambao zamani ulikuwa ngano, kaokwa kuwa mkate, na

akaumega na kuuning'iniza huko nje kwa . . . akautoa kwa watu, na ulirudi tena. Kazidisha kiumbe!

102 Lakini katika siku za mwisho, ambapo hakuna ishara ya kiumbe, Yeye hukinena na kikaumbika, kwa vyovyote, ikionyesha kuwa ndiye Mungu yule yule aliyekuwa mwanzoni. Yeye anaweza kuumba kindi, Yeye anaweza kuumba chochote Yeye atakacho, kwa sababu Yeye ni Mungu. "Mambo makubwa kuliko haya mtafanya, kwa kuwa naenda kwa Baba Yangu." Neno halikosei na halina budi kudhihirishwa na halina budi kutimia. "Kubwa kuliko hili mtafanya," si kuzidisha, bali kukinena hata kikaumbika.

103 Angalieni katika Neno sasa Yeye alipoahidi. Tuko wapi, wapi basi? Tunaishi siku gani? Ni wakati gani? Kudhihirishwa kwa Neno la Mungu kama ilivyo katika nyakati zote. Mna Ujumbe juu ya *Nyakati Saba za Kanisa*. Angalieni hasa jinsi kila mmoja wa wale wanyama waliotoka nje, na Wanyama waliowafuata hao. Angalieni sawasawa ikiwa haikutukia kupitia wakati wa wale watengenezaji, na kila wakati, sawasawa tu na njia ilivyokusudiwa iwe, jinsi hasa Neno lilisema. Na vivyo hivyo Roho Mtakatifu atadhihirisha leo sawasawa tu na kile Biblia ilichosema kingalikuwa.

104 Tunaona kivuli cha angani ardhini, na mambo yote, na baraza na kadhalika yakiwa tayari.

105 Na tunaona, katikati ya hayo yote, Injili yenye utukufu ya Yesu Kristo, iliyoahidiwa kwa ajili ya siku hii, ikijidhihirisha Yenyewe. Tunaishi katika wakati wa ajabu. Shalom kwenu ambao mna Neno kwenye vilindi vya mioyo yenu, mliochaguliwa kabla kuwekwa misingi ya ulimwengu, kulisikia Neno la siku hii. Kama husikii, kwako mwaka ujao ni mbaya. Kama wasikia, kwako ulimwengu ujao ni mkuu, ama siku kuu, mwaka mkuu unaokuja sasa, mwaka mpya.

106 Si kugeuza ukurasa mpya; watu wengi hujaribu kugeuza ukurasa mpya kwenye mwaka mpya, wakaugeuza tena siku ifuatayo.

107 Kama hadithi dogo niliyokuwa nikisoma hivi majuzi asubuhi. Mwanamke mmoja alimpazia sauti mumewe, aliyeamka mapema akaenda akanunua gazeti la asubuhi, na alikuwa analisoma hilo gazeti la asubuhi. Alisema . . . Mwanamke huyo alisema, "Kuna chochote kipya katika habari?"

Yeye alisema, "Hata, ni jambo lile lile tu, ila watu tofauti."

108 Hivyo ni kama ilivyo leo, kitu kile kile. Tuna dhehebu jipya, fundisho lile lile la kale; linapembelezwa-pembelezwa tu, mtu fulani apate sehemu yake dogo kuelekea upande *huu* au upande *ule*.

109 Hii ni siku mpya! [Ndugu Branham anagonga mimbarani mara mbili—Mh.] Haleluya! Hii ni siku ambayo tunapaswa kuondoka na kuangaza, katika Nguvu za Yesu Kristo. Giza kuu likitulia juu ya dunia; kunapaswa kuwa na siku mpya kwa ajili yetu, naam, kweli, akilifanya tu jinsi Yeye hulifanya. Lakini ligeukieni Neno Lake na muone ahadi ambayo imeahidiwa kwa ajili ya siku hii, na mtajua kama mnaishi katika Nuru au la. Kubadilisha kalenda hakubadilishi wakati; inabadilisha kalenda tu.

110 Sasa sikizeni kwa makini. Fanyeni kama Daudi alivyofanya, wekeni ya usoni mkononi Mwake. "Vipi? Nitajuaje la kufanya, Ndugu Branham?" Weka ya usoni mkononi Mwake. Haidhuru kijacho au kiendacho; mtumaini Yeye. Yeye ni Neno, jua sasa. Daudi alisema, "Wakati Wake u mkononi Mwangu. Mtumaini Yeye daima. Daima mtumaini Yeye." Alijua ni Nani aliyeshikilia ya usoni, Daudi alijua, hiyo ndiyo sababu angalisema hili. Kuna Mmoja tu ashikiliaye ya usoni; huyo ni Mungu. Kwa hivyo, Yeye hushikilia ya—ya usoni, mwache Yeye akushikilie. Sawa.

111 Baadhi ya watu husema, "Lakini, Ndugu Branham, Mimi nimejaribu nikajaribu."

112 Lakini ngojea dakika moja. Subira yavuta heri. Subira ni heri ya Roho Mtakatifu. "Wamngojeao Bwana watapata nguvu mpya."

113 Unasema, "Ninawezaje kungojea zaidi?" Endelea tu kungojea. Uishapo kutenda yote uwezayo kutenda upate kusimama, basi simama, waona, simama tu. "Nitalifanya jinsi gani?" Simama! Yeye alisema ni Kweli, na ni Kweli. Yeye alisema itatendeka. "Vipi?" Sijui; bali itatendeka. Yeye alisema hiyo. Yeye aliiahidi. Kama Yeye aliiahidi itatendeka. Hayo tu. Haiwezi kuharibika.

114 Kwa hivyo sasa kumbukeni, ilimchukua Mungu maelfu ya miaka kutimiza ahadi yake ya Mwokozi ajaye. Ilimchukua Mungu miaka elfu nne kutimiza ahadi hiyo. Lakini Yeye alijua, tangu mwanzo, ni lini hasa itakapotukia. Yeye alijua; hukuna mwingine aliyejua. Yeye alisema tu itatukia. Na ilipotukia, watu walikuwa wamedanganyika sana hivi kwamba hata hawakujua jinsi ya kuikubali. Jambo lilo hilo limejirudia tena! Hufanya hivyo daima, halikosi, pande zote mbili, daima.

115 Yeye alifanya nini mnamo miaka hii? Yeye alionyesha mifano ya kuja Kwake.

116 Yeye alionyesha hilo katika Yusufu. Kama mngeangalia maisha ya Yusufu; alichukiwa na ndugu zake, alipendwa na baba yake. Kwa nini? Kwa sababu alikuwa wa kiroho, kwa sababu aliona maono. Wale wengine hawakuona maono; wao walikuwa wazee wetu bali hawakuona maono, kutafsiri ndoto. Lakini walimwonea wivu. Naye aliuzwa karibu vipande thelathini vya fedha, akainuliwa kutoka shimoni ambamo alikusudiwa

kuuawa, akaketi kwenye mkono wa kulia wa Farao. Na alipoondoka kwenye kiti cha enzi, tarumbeta ililia, “Pigeni magoti; Yusufu anakuja!”

117 Sawasawa tu na kile Yesu alichotendewa, huketi mkono wa kulia wa Mungu. Na Yeye atakapoondoka kwenye Kiti cha Enzi, tarumbeta zitalia. Na kila goti litapigwa, na kukiri kwa Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Sawasawa.

118 Yeye alilionyesha kwa mfano wa Daudi, alipokuwa juu ya . . . mfalme aliyekataliwa akiutazama Yerusalemu, akilia. “Mara ngapi nimetaka kuwakusanya, kama vile kuku avikusanyavyo vifaranga vyake, wala humtaki.”

119 Kote katika wakati, Yesu alionyesha kwa mifano, akijua ya kwamba siku moja mfano wa mwisho utatimizwa, na kudhihirishwa kamili kwa Masihi Wake aliyeahidiwa kungekuwako. Na ahadi kamili ilipokuja, ingawaje Yeye alitoa mifano yake . . . Siku baada ya siku, mwaka baada ya mwaka, Yeye alitoa mifano Yake. Na ilipofikia ukweli wake, hawakuiamini.

120 Yeye ameisha fanya jambo lilo hilo, kuitoa kwa mfano, na kuionyesha katika nyakati za kanisa, na kila kitu, hadi wakati huu tunamoishi, na watu wako katika giza kuu, yaonekana kama kwamba hawawezi kuielewa tu. Jambo la huzuni sana!

121 Si zaidi ya kuona kijana mwanamume kule nje, mwema, mkubwa, ameumbika vizuri na nywele zake, ambazo huzisokota kama wafanyavyo wanawake, amevaa mavazi yenye kumbana, na sweta ndefu inayoning’inia chini, na viatu vya zambarau. Ni wa kiume? Lo, jamani, ni kitu cha kutisha jinsi gani kukiita mwanamume! Ni kitu cha namna gani kukiita mwanaume! Hiyo ni kweli.

122 Mnaona mwanamke fulani, anayedhaniwa mrembo na wa kuvutia, anatokea akivaa suruari ya mwanamume, sigara mdomoni, na nywele imekatwa. Ni kitu cha namna gani kuitwa mwanamke! Yesu alimwita Mariamu, “mwanamke.” Hapaswi kuitwa mwanamke, utu uke tu.

123 Tazameni, na wakati! Kwa nini? Pengine watu wanaodai na kudhani wana moyo safi, lakini giza kuu limeisha waingiza katika hili. Biblia ilisema wangalikuwa hivyo. Soma Isaya 6 na uone kama wanawake hawangefanya hivyo siku za mwisho, sawasawa tu na kile Biblia ilichosema wangekuwa. Ni Neno la Mungu. Yeremia na wengineo walinena juu ya wakati huu tunamoishi sasa, kwa sababu waliuona mwisho tangu mwanzo. Kwa hivyo tunayaona mambo haya, na giza kuu juu ya watu.

124 Ndio, ilimchukua Mungu maelfu ya miaka, tupa . . . akionyesha mifano na kila kitu, na mwishowe wao hawakumjua Yeye alipokuja, ingawa Yeye alionyeshwa katika Yusufu na Daudi na Eliya, na kupitia kote kote huko. Yeye alionyeshwa nao, na bado hatuwezi kuelewa kwa nini hawakuiona. Na pale

ulikuwa, papo hapo Maandikoni, “Kutoka Bethelehemu ya Yuda,” Yeye angezaliwa. Tunaona hayo katika Maandiko jinsi Yeye angezaliwa, bikira. “Bikira atachukua mimba na atazaa Mtoto, na watamwita Jina Lake Imanueli.”

125 Kwa nini wao walimuua Yeye? “Kwa sababu Yeye alijifanya Mwenyewe kuwa Mungu,” naye alikuwa Mungu. Hakika, wao hukubali hilo. “Yeye alisema alijifanya Mwenyewe kuwa Mungu, sawa na Mungu, akisema, ‘Mimi ni Mwana wa Mungu.” Naam, Yeye alikuwa hivyo!

126 Biblia ilisema anapaswa kuitwa, “Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, Wa Ajabu!” Hivyo ndivyo Yeye aliyokuwa. Kwa nini wao hawakufahamu hayo?

Sio ajabu Yeye alisema, “Yawapasa myachunguze Maandiko.”

Wao walisema, “Sisi tu wanafunzi wa Musa.”

127 Kasema, “Kama mngalikuwa wanafunzi wa Musa, mngalinijua Mimi. Musa aliandika juu yangu.” Nao hawakujua hilo.

128 Na wakati umewajilia watu tena, ambapo wataziendea kanuni zao za imani na kadhalika, badala ya mpendwa Yesu. Hiyo ni kweli. Mambo haya makuu yanayokuja, na yanawaingiza moja kwa moja kwenye giza zaidi na zaidi. Na Mungu analitangaza katika Neno Lake, kwa ishara na maajabu angani, na kuendelea kuonyesha, akinena mambo ambayo hutendeka sawasawa tu na saa na dakika, ambayo yangetimia. Na hata hivyo wao huendelea mfululizo na njia ile ile. Yaonekana kama wao hawawezi kujimudu. Watu wema, naam, bwana, wakifanya jambo lile lile leo kama walivyofanya wakati ule.

129 Sisi ni viumbe vya wakati. Mungu ni viumbe vya Milele . . . Mungu ni kiumbe cha Milele. Yeye hakuanza kamwe wala hatakwisha kamwe. Kwa hivyo mbona usijikabithi tu Kwake? Tazama juu, na uangaze na furaha ya Nuru ya Neno la Mungu ambalo linaangaza leo. Kwa nini watu hawawezi kuona Hilo, marafiki?

130 Sikilizeni, mimi ni ndugu yenu. Nawapenda. Si ingalikuwa rahisi kwangu mimi kuvumilia tu, iwapo, na kuendelea na kusema, “Lo, vema, nitapatana juu ya Hili, nitapa . . . ”? Mimi si kuundwa kwa hicho. La, bwana. Iwapo ni Neno, ni Neno. Mungu atusaidie sisi tusimame kwa ajili ya kitu kilicho kweli! Naam, bwana. Ingekuwa sawa, hakika, ungepata pongezi zaidi. Lakini mimi, nitafanya nini pale Siku ile huku vile vidole vyembamba vikielekezwa usoni mwangu na kusema, “Wewe ulijua bora zaidi, bali ulishindwa kutuambia sisi”? Whiu! La!

131 Nitakuwa kama Paulo, “Sikujiepusha na kuwahubiria habari ya kusudi lote la Mungu.” Hamna damu ya mtu juu

yangu. Hebu liende popote liwezapo kuwa. Hiyo ni Kweli. Mungu anaijua, na Yeye anaiunga mkono na kusema ni Kweli.

132 Tugeukie nini, Ndugu Branham? Ninyi, ninyi mngekuwa wapumbavu kufanya jambo kama hilo. Mgeukieni Kristo, na Yeye ni Neno! Mgeukieni Kristo!

133 Msikaribie kanuni za imani! Rudini katika . . . Sijali, waweza kuwa ulianza kanuni yako ya imani, miaka mia tano iliyopita, kwamba wewe tu . . . Hilo halimaanishi kitu kwa Mungu. Hao Masadukayo na Mafarisayo walianza kitambo kabla hujaaza, na walihukumiwa.

134 Lo, mnajaribu kuweka bayana ya Roho Mtakatifu juu ya vitendo tofauti. Ninaamini madhihirisho ya Roho Mtakatifu. Yanafanya nini? Mpentekoste husema, "Kunena na lugha ndio bayana ya kwanza ya Roho Mtakatifu." Nimeisha waona wachawi na walozi wakinena kwa lugha. Nimeisha waona wakinena kwa lugha na kunywa damu toka kwa fufu la kichwa cha mwanadamu, na kutabiri na kukanusha kuna kitu kama Mungu. Nimeisha kuwa kwenye kambi za wachawi ambako wanaweka kalamu juu ya meza na kuifanya irukaruke juu chini, na kuandika katika lugha isiyojulikana. Hiyo ni kweli. Hilo halina jambo la . . . Hata hivyo naamini Mungu hunena katika lugha sizizojulikana kupitia watu Wake. Lakini mnatia mkazo zaidi juu ya hilo, "Kwa nini pasiwe na mtafsiri? Kwa nini wapaswa uwe ujumbe kwa kanisa?"

135 Basi ninyi watu wengine, mnasema, "Matunda ya Roho, hivyo ndivyo tunajua. Upendo, furaha, hivyo ndivyo tunapata bayana." Ndivyo? Basi Christian Science wamewashinda ninyi nyote. Wao wanajizoeza hayo zaidi kuliko nyinyi nyote Wapentekoste, Wamethodisti, na Wabatisti, mkiwekwa pamoja.

136 Chunguzeni kile kitendekacho. Hebu niwaonyesheni ninyi matunda ya Roho, na muone kama mngaliweza kuendea hayo tena. Hebu na tumchukue Yesu. Mungu anisamehe kwa ajili ya maneno hayo niendayo kusema; nitakuwa dhidi Yake kwa dakika moja, kuwaonyesheni, twaeni baraza hizi za watu hapa, na baraza hili la watu hapa adhuhuri hii. Nitasema . . .

137 "Mabwana, kuna kijana hapa, Jina Lake Yesu wa Nazareti, msijishughulishe Naye kwa kitu chochote! Nani aliyekuwa wa kwanza . . . Biblia yetu hutufundisha nini? Mungu ni upendo. Nani aliyekuwa wa kwanza kuja ulipozaliwa? Kasisi wako wa kale mwenye fadhili. Hiyo ni kweli. Nani aliyekujia ulipokuwa mhitaji, hukuwa na pesa, na akakukopesha pesa? Kasisi wako wa kale mwenye fadhili. Sawasawa. Nani aliyewekelea mkono wake mabegani mwako, na mabegani mwa mama yako, mlipokuwa karibu kutengana, na kuwaombea mumrudie Mungu? Kasisi wako wa kale, mwenye fadhili. Nani aliyeungana nawe, mlipoteta, wewe na jirani yako, na kuwarudisheni tena ushirikani? Kasisi wako wa kale, mwenye fadhili. Hiyo ni kweli.

Ni nani, atakayesema maneno ya mwisho juu yako katika siku ile huko ng'ambo? Ni nani? Wanakuacha ulale pale na kuoza; bali kasisi wako wa kale, mwenye fadhili, huja na kukubariki, na kulituma Neno la Mungu pamoja nawe. Kasisi wako wa kale, mwenye fadhili!

138 "Ni vipi kuhusu huyu Mtu anayeitwa Yesu wa Nazareti, basi, mnaona, Yeye alitoka shule gani? Kasisi wako wa kale, mwenye fadhili, ilimbidi kutoa dhabihu maishani mwake mwote. Babu yake alikuwa kasisi. Babu wa babu wa babu wa babuye alikuwa kasisi. Alitumia wakati wake wote katika dhehebu. Yeye amefundishwa Neno; anajua kile anachonena."

139 Sasa tunazungumza juu ya matunda ya roho: fadhili, upendo, furaha, amani, ufahamu, uvumilivu, subira, mnaona, tunda la Roho.

140 "Na huyu Yesu je, Yeye alitoka wapi? Hatuna neno kwamba Yeye ametokana na shule iwayo yote. Yote Yeye atendayo ni kuvuruga shule ambazo tumeisha jenga." Hamna tunda la Roho sana, sivyo?

141 "Yeye alifanya nini ng'ambo kule ambapo hao wachuuzi maskini chini huko, na wafanyi biashara ambao iliwabidi ku . . . Wao, wao hawafugi kondoo, kwa hivyo wao—wao walitengeneza zizi dogo pale ili watu wapate kuleta kondoo. Yule mfanyi biashara maskini, yeye—yeye anataka kutoa sadaka ya kondoo, kwa sababu ni matakwa ya Mungu. Yeye anamleta yule yule kondoo, kumuuzia mfanyi biashara, ili kwamba apate kutoa sadaka kwa ajili ya nafsi yake. Amefanya nini huyu Yesu wa Nazareti? Alipiga teke meza zake; akatwaa ngozi na kuisokota pamoja, kawapiga na kuwafukuza hao makasisi mle; na alimwita kasisi wako wa kale, mwenye fadhili, 'nyoka nyasini; mnafiki'!"

142 Sasa mnaita hilo tunda la Roho? Hakika sivyo. Basi tunda lako la Roho linaangukia wapi? Si zaidi kuliko unavyodhani juu ya huruma, huku akipitia katikati ya umati wa watu kule, umati wa watu wakilala, vipofu, viwete, walioteseka, waliopooza, wanaochechemea, vilema, na kamwe hakumponya hata mmoja wao; akijaa huruma. Watu wenye nia ya mwili hawatalijua kamwe. Seminari hazilifunzi. Ni ufunuo. Hakika. Tunda la roho huanguka kutoka humo, sivyo? Hao makasisi walikuwa na tunda la Roho mara kumi.

143 Ungejuaje kilicho sahihi? Dhihirisho la Neno lililonenwa la Mungu likidhihirishwa, Nuru ya wakati. Bila shaka. Hiyo hapo bayana ya Roho Mtakatifu, kuamini Neno la Mungu linapodhihirishwa. Yeye alikuwa Neno, lililodhihirishwa. Na baadhi yao walililikana, wakalichekea, wakamdhihaki na kumwita Yeye m—mpiga ramli, roho mchafu; ndiyo hiyo hapo ile bayana, kunena kwa lugha, ndiko bayana ya yale matunda. Bayana ya pekee iliyopo ni, ni mtu aaminipo Neno lililoandikwa.

Linapothibitishwa, anatembea katika Nuru Yake. Yesu alikuwa Nuru ya wakati ule kwa sababu alikuwa Neno lililoahidiwa kwa wakati huo, na alijaribu kuwaambia hivyo, lakini walikuwa zaidi—zaidi gizani kulielewa. Hivyo ndivyo ilivyo, leo, sasa.

144 Sasa tu viumbe vya wakati. Mkabidhini Yeye njia zenu, Naye atayaleta ya usoni sawa, kwa sababu tunamuona Yeye tu vile alivyo katika Neno.

145 Mmemwona Yeye akilithibitisha Neno lililoahidiwa kwa ajili ya leo. Mnaliona katika ishara mwezini. Mnaliona makanisani. Kumbukeni.

146 "Ulisema, 'kanisani,' hilo linahusu kanisa vipi?"

147 Ngoja kidogo tu. Mwezi huwakilisha kanisa. Yerusalemu ndio mji wa kanisa wa zamani sana unaojulikana duniani. Melkisedeki alitoka mji huo; Mfalme wa Salemu, Mfalme wa amani, Mfalme wa Yerusalemu. Hiyo ni kweli, mji ulio wa zamani sana duniani. Na huo ulikuwa mwezi, kama pale torati ilipobuniwa, na hapa laja hili wimbi la giza la Mataifa likija juu yake. Yeye alisema, "Wao, kanisa lingalikanyaga kuta za Yerusalemu hata majira ya Mataifa yatakapotimia." Na liko hapa. Tunaishi ndani yake. Linarudi moja kwa moja nyuma, kweli tu kama vile jina langu ni William Branham. Naam, bwana, tunaweza kuliona. Limetiwa kivuli, lilionyeshwa kwa fumbo mbeleni, lilitabiriwa; kuitwa kwa Wateule watoke. Wao wanapapasapapapasa moja kwa moja gizani, wengine wao, wanapoendelea. Naam.

148 Sasa tunaliona Neno Lake likithibitika. Tunaamini kwa hivyo ikiwa Yeye alilithibitisha Neno la leo, kile lilicho, ninajali nini kuhusu kile mwaka uletacho? Ninajali nini kuhusu mwaka ujao? Ninajali nini kama ninaishi leo au nife leo? Kila Neno ambalo Yeye aliahidi litathibitishwa, kila moja! Ikiwa Yeye anaweza kulifanya leo, baada ya kuliahidi miaka elfu mbili iliyopita; ikiwa ni miaka elfu mia moja, leo, Yesu atarudi duniani katika mwili unaoonekana, kwa ajili ya Kanisa, li—lililokombolewa, Bibi-arusi, na kumwondosha hapa. Si hoja ni nini kijacho, kiendacho, mitindo, ikisema "endelea," na watu wanaweza kuenda kwa shida katika giza tupu na kuamini chochote wanachotaka kuamini, bali Yesu Kristo atarudi tena. Namkabidhi ya usoni, basi. "Bwana Mungu, sijui kesho inashikilia nini, bali ninajua Wewe unashikilia kesho."

149 Neno Lake ni kama tu muziki mkuu wa taarabu. Ni wangapi wenu wamewahi kusikia taarabu? Vema, kila mtu amepata kusikia. Sasa kumbukeni, taarabu ni wakati muziki unachezwa kama mchezo wa kuigiza. Nadhani nimepata hilo sawa, taarabu. "Petro na Mbwa Mwitu," mnakumbuka hiyo, hadithi ya kale jinsi walivyozoea ku. . .nimeisha usikia huo, jinsi wanavyotwaa ngoma na kufanya kama yule—yule kigogota mdogo akigota, na

Petro akitoka nje, na kunguruma kama mbwa mwitu, kule kulia kwa baragumu; muziki wa taarabu.

150 Sasa, ikiwa huelewi taarabu, ni ghasia tupu kwako, kama huelewi. Inakubidi uelewe ni nini. Yote hufanywa kwa ishara na miendo, bali hufanywa kama mchezo wa kuigiza. Sasa, tunatambua, mtu pekee aelewaye taarabu ni mtungaji, na wale ambao wana hamu ya kufahamu, hujua mabadiliko yake, hujua kinachotendeka.

151 Mtungaji hujua kila mwendo, tangu mwisho hadi mwanzo, tangu mwanzo hadi mwisho. Ulijua hilo? Yule tu aliyeliandika, yeye huutunga huu, yuajua kila kiungo kidogo. Kama yuajua kila kiungo, yambidi kiongozi kuwa vivyo hivyo, kuuongoza. Sasa utaenda kugeuza jinsi gani kanuni zako za imani katika hilo? Kukosea pigo la ile fimbo, ishara hiyo, kukosea kidogo kwa kiungo, kungetupilia taarabu yote mbali, hutupilia mbali muziki wote, hutupilia taarabu yote kwa jumla. Sasa mnajua hiyo ni kweli. Mtungaji na kiongozi hawana budi kuwa katika roho yule yule.

152 Hiyo ndiyo sababu mhudumu na Neno la Mungu, Taarabu kuu ya Mungu aliyokuwa akicheza tangu mapambazuko ya wakati; mhudumu, Nenoni, hahitaji kuangalia juu hapa na kusema, "Naamini *hili* lapaswa kuwa; yakupasa kulifanya kwa njia *hii*." Inambidi kuenenda jinsi ukurasa wa muziki usemavyo auendee. Hivyo ndivyo Injili inabidi kuhubiriwa, jinsi Neno lisemavyo ichukuliwe. Unajua, kama ungetupa kanuni za imani mle, ungechafua kitu chote kwa jumla. Inapaswa kuenda kuufanya mchezo wa kuigiza kuwa sawa kabisa.

153 Kiongozi anapaswa kuenda vile mtungaji alivyosema, kuucheza vilivyo, huo muziki. Sasa tazama, yote yanafanywa kwa ishara, na inapaswa kuwa sauti inayofaa.

154 Paulo alisema, "Baragumu ikitoa sauti isiyojulikana, ni nani atakayejifanya tayari kwa vita?"

155 Sasa mnamwona Mtungaji, Mungu aliyeandika Biblia, yote pamoja ni ufunuo wa Yesu Kristo. Yeye anajua mabadiliko ya wakati. Na mtu yule, yule—yule kiongozi ambaye anawaongoza, ishara ya wakati, yampasa kuambatana kabisa na ishara za Biblia. Haleluya! Jamani, jamani, jamani, jamani, jamani!

156 Loo, ndugu, dada, ulimwengu una nini? Kwa nini nimeenda kichaa? Kuna kasoro mahali fulani. Taarabu hailingani kwa sauti na ukurasa wa Muziki! Wanabuni kanuni za kanisa na mengineyo, ambapo ni Neno linalohitajiwa kuhubiriwa, kudhihirishwa. Viongozi wana walakin, kisha kundi lote kwa jumla limechanyikana, wasijue la kufanya. Wote ni wenye matata, "Nini kilitendeka? Kwa nini *hili* lingefaa? Kwa nini, *hili* kutendeka? *Hili*, hilo lilitendeka vipi?" Kisha hawajui la kufanya sasa. Wanatawanyika, kwa sababu haijalingana na Neno. Hiyo ndiyo hoja ya kile tunachoita, ufufuo wa siku za mwisho. Hiyo

ndiyo hoja ya ujumbe wetu wa Kipentekoste. Tumetoka kwenye kipimo cha muziki wa Biblia, tuliondoka tukaenda kuunda dhehebu kama walivyofanya huko nyuma. Limetoka nje ya kipimo cha muziki.

157 Mungu, turehemu. Laiti ningalikuwa na maneno ya kulifanya lididimie kilindini, kama tusemavyo, nipate kulitandaza wazi na kulimwagilia ndani.

158 Hauwezi kuona, ndugu yangu, dada, inapaswa kuwa katika ulinganifu wa sauti. Yampasa kiongozi kuwa pamoja na Neno. Lisemapo jambo moja, usiseme jambo lingine; itatoa ishara baya, kisha jambo lote kwa jumla linatoka katika mdundo. Hiyo ni kweli. Neno la Mungu ni huruma kuu, taarabu, hasa, samahani. Huna budi kuanza kama alivyofanya katika muziki. Huna budi kuanza pamoja Naye. Angalia, ingia katika mdundo Wake.

159 Wasema, "Vema, nilijiunga na kanisa." Huo sio mdundo. "Nilifanya hivyo." Huo sio mdundo. "Nilienda hata madhabahuni na ni—nikasema, 'Ninaamini Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu." Shetani hufanya vivyo hivyo. Huo sio mdundo. Unaona, unakosa njia. Nini kilitendeka? Huenda ikawa kiongozi fulani alikuambia, "Salimiana kwa mikono na uandike jina lako kitabuni; jiunge na kilabu chetu, dhehebu letu." Ninyi nyote mmekosea njia!

160 Kisha jambo halisi lianzapo kutendeka huko nje miongoni mwa kundi dogo, utasema, "Vema, na *Hilo* je, wako nje ya ulinganifu" Rudini kwa Neno na muone ni nani aliye nje ya huo ulinganifu. Oneni kile Mungu alichoahidi. Oneni kile Mtungaji alichonena juu yake.

161 Mnaona, mna kila mtu katika wasikizi wenu. Hiyo ndiyo sababu ulimwengu unaangalia kila mahali. Wakati kanisa linapaswa kutazamwa kama nyota yenye kung'aa na kuangaza, Taa iliyo juu ya kilima, ambayo hakuna mtu anayeweza kuishinda kuangaza, hakuna mtu wa kuihukumu.

162 Na, leo, linachekelewa na ulimwengu, kwa sababu viongozi wamelitoa nje ya ulinganifu wake na Mtungaji. Mnaona ninachomaanisha? Wanacheza mambo ambayo hayamo mle. Wanamuziki hawajui lakufanya hata kidogo sasa; kanisa, wote wamepotoka. Tumekuwa tukizungumza kuhusu ghasia hii yote, miaka yote, na kuilaumu, na sasa wanaungana moja kwa moja nayo. Loo, kuna kasoro mahali fulani.

163 Angalieni, sharti muanze katika Muziki kama Yeye alivyofanya, ingieni kwenye mdundo Wake, ingieni katika Neno lililoahidiwa. Oneni jinsi yeye alivyoifanya hapo mwanzo, Oneni jinsi Yeye alivyoifanya katika zile nyakati za katikati, oneni jinsi aifanyavyo sasa, sawasawa daima.

164 Mchunguze kiongozi, jinsi yeye aifanyavyo. Kama haifanyi, kama anakuelekeza kwenye dhehebu fulani, hakujakuweko

kamwe na kiongozi aliyefanya hivyo. Kiongozi daima alikuelekeza kwa Neno. Manabii wa kale, walielekeza kwa Neno. Wao walikuwa Neno. Walililiishi Neno. Na lilifanya nini? Lilimdhihirisha Mungu. Hilo lililifanya hai Neno lililoandikwa kwa ajili ya siku hiyo, kwa sababu liliwajilia wao. Lilifunuliwa kwao. Huo ulikuwa Mwamba wao. Haleluya!

165 Yesu Kristo, Neno la Mungu, ni Mwamba wetu. "Juu ya Mwamba huu nitalijenga kanisa Langu," Neno lililofunuliwa la Mungu. Shalom, kwa mwaminio halisi. Amani! Tuko katika wakati wa mwisho. "Juu ya Mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu," Ufunuo wa Neno.

166 Mmoja alisema, "Vema, u Mtu mkuu, Wewe ni kama Musa. Wewe u Mtu mkuu. Wewe ni kama . . . " Hilo silo.

Lakini ufunuo ulisema, "Wewe ni Mwana wa Mungu."

167 Kasema, "Mwili na damu havikukufunulia Hili, bali Baba Yangu aliye Mbinguni. Juu ya Kweli hii iliyofunuliwa nitalijenga Kanisa Langu."

168 Nini? Yeye ni Neno. "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, Naye Neno alikuwako kwa Mungu, Naye Neno alikuwa Mungu," Naye Neno angali Mungu. Yeye tu, aliye yule leo, akijidhihirisha Mwenyewe jinsi alivyokuwa; Musa na Eliya, kote kote, na Yesu, na Mungu yule yule leo, inamfanya Yeye "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele," Waebrania 13:8. Mnaona, hawakuwaelekeza ninyi kwa kundi fulani. Waliwaelekezeni ninyi kwa Mtu, waliwaelekezeni ninyi kwa Neno, Mungu.

"Nianzie wapi, Ndugu Branham?"

169 Msalabani, anzia Msalabani pamoja Naye. "Tubu, liamini Neno," hivyo ndivyo Biblia ilisema. Kisha fuata kupitia kwa mdundo wa Neno lingine lote.

Unasema, "Vema, nitafanya nini?"

170 Endelea tu kuufuata mdundo wa Neno. Ikiwa "kutubu" ndilo jambo la kwanza, katika kulitambua, fanya hivyo, hiyo ndiyo hatua yako ya kwanza. Weka hatua yako ya pili pale Neno lisemapo. Kuendelea, na kuendelea, na kupiga hatua taratibu Naye.

171 Usiuvunje mdundo ikiwa u sehemu ya taarabu ya Mungu. Usiuvunje mdundo wa Neno. Usiulize, "Vema, kwa nini? Kwa nini *hili* lilitendeka? Nililijaribu, Ndugu Branham, na, waliponifukuza, unajua nililofanya? Niliona njaa nusura nife." Usiulize kwa nini. Yeye anajua mdundo, jinsi unavyopaswa kubadilishwa, na ni kiungo kipi unachopaswa kufanya, naam, bwana, kwa sababu umeandikwa. Yeye anajua yote juu Yake. Yeye anajua mdundo. Usiulize kwa nini. Uamini!

172 Mungu ametembea kupitia kote katika wakati wa historia, pamoja na Neno Lake lililoahidiwa, kwa kila wakati, na kamwe hajashindwa (kukatiza) mdundo, kwa Nguvu za Mungu,

inapowafikia walioteuliwa na watu waliothibitishwa. Mdundo wa Neno Lake katika siku za Nuhu, mdundo wa Neno Lake katika siku za Nuhu, katika siku za Musa, katika siku za Eliya, katika siku za Yohana, katika siku za Daudi, katika siku za Yesu, na kuendelea. Yeye hudumisha mdundo wa Neno, kuendelea moja kwa moja, hajawahi kuukatiza kamwe. Yeye amekuja kupitia kote katika historia. Na Mzao aliyeteuliwa, ambaye aliliona na kuliamini, huingia moja kwa moja kwenye mdundo huo pamoja nalo.

173 Wale wengine husema, "Vema, lakini kanisa husema..." Hilo halina uhusiano wowote Nalo. Hukuzaliwa kufanya hilo.

174 Umezaliwa katika Neno, kwa kuwa umezaliwa katika Kristo. Kristo ni Neno, naam, bwana, kila moja katika wakati wake.

175 Unasema, "Vema, nitakuambia tu, Ndugu Branham, mimi siwezi kuangalia mbele."

176 Basi angalia juu. Mungu aliahidi, kama ungeangalia juu, ungemwona Yeye; shalom, amani, amani ya Mungu ikupumzishe.

177 Unasema, "Basi mbona watu wengine hunifanyia mzaha, Ndugu Branham? Unajua, watu wengine hunifanyia mimi mzaha, na kusema mimi—mimi nina 'nywele ndefu', mimi ni 'wa mtindo wa kale,' kwa wanawake." Mwanaume, "Kwa sababu ninaamini Biblia, 'Huna ushirika nasi tena. Hatuwezi kukukubali kwa sababu ya—ya kuwa unaamini kitu *fulani na fulani*.'"

178 Na unajua ni sawasawa na jinsi Neno limeandikwa. Mungu anawajibu kwako, kuunga Hilo mkono wakati huo. Yeye anao bila shaka. Usijali hilo, kwa nini wao husema lifanyiwe mzaha. Mungu ni Mungu mwenye wivu. Kumbuka kuteseka kwa ajili ya Neno Lake ni maumivu ya kukua kwa neema Yake. Unapoteseka kwa ajili ya Neno Lake, ni maumivu tu ya kukua.

179 Unajua jinsi mtoto mdogo, wa umri wa miaka kumi, kumi na mbili, anavyoumia. Huingia, kasema, "Mama, mikono yangu yauma na miguu yangu inaniuma," na kadhalika. Ni maumivu ya kukua. Yaonyesha ameishapata vitamini fulani nzuri. Yeye anakua.

180 Na mtu fulani aanzapo kukufanyia wewe mzaha, aseme, "Ni mwanamke wa mtindo wa kale. Mtazame, yeye ni...Loo, nitakuambia, alizoea ku..." Sawa, kumbuka tu, ni maumivu ya kukua. Hiyo ni dhuluma iliyo nzuri kwako. Ni maumivu ya kukua.

181 Loo, naam, Yeye huachilia misalaba na njia panda na viungo. Yeye hufanya hivyo daima, ili atukamilishe kwa huduma Yake. Yeye huachilia mambo hayo yatendeke. Hamwezi kufahamu hilo? [Kusanyiko lasema, "Amina."—Mh.] Yeye hufanya hivyo

ili apate kuwakamilisha ninyi kwa mwito aliowaitia. Hayo ni maumivu ya kukua kwenu. Yeye alimfanyia Daniel hivyo, mwajua.

182 Yeye aliwafanyia hivyo watoto wa Waebrania, katika tanuru ya moto. Tanuru ya moto ilifanya nini? Tanuru ya moto ilivunja tu kamba zilizowafunga. Hayo ndiyo tu tanuru ya moto iliyofanya, ikateketeza tu zile kamba.

183 Wakati mwingine inahitaji majaribio kukata kamba za ulimwengu kutoka kwetu, kukutoa wewe ulimwenguni. Huenda ikawa, yanapaswa kukutoa nje ya kanuni yako ya imani, kwanza. Kama mtu anayezama mtoni, yakupasa umtoe mtoni kabla haujatoa mto katika yule mtu. Hivyo ndivyo karibu njia inampasa Mungu kutenda jambo. Acha wao wakutupe nje, mara moja, kisha watautoa ulimwengu toka kwako. Yawabidi—yawabidi kukutoa katika ulimwengu, kwanza. Wakati mwingine haya maumivu ya kukua ndiyo yanayofanya hayo. Lo, naam.

184 Mungu husimama juu ya Neno lililoahidiwa kwa ajili ya kila mwaka mpya. Yeye husimama juu yake, mwaka huu, kutimiza kile Yeye alichoahadi kwa ajili ya mwaka huu. Chochote kile, mimi nataka kuwa kabisa katikati ya mapenzi yake siku za usoni, kama walivyofanya.

185 Kama Ibrahimu, alipokutana na njia panda zake, hakujua jinsi angalitenda. Mungu alimwambia, "Nitakupa wewe mwana." Alingojea kwa miaka ishirini na mitano. Mwishoni mwana akaja, kisha Mungu alisema, "Sasa, kwa mwana huyu, Mimi nitakufanya wewe baba wa mataifa mengi. Mchukue juu kule ukamuue. Mchukue ukamuue," aangamize kitu kile kile ambacho alikingojea miaka ishirini na mitano. "Mtwae ukamuue."

186 Ibrahimu hakufadhaika kamwe. Haikumsumbua kamwe. Alitwaa kuni na kuziwekelea juu ya maskini punda mmoja, kisha akamchukua mwanawe. Kampleleka kwenye kilele cha kilima, kumtoa sadaka, kwa sababu Ibrahimu alijua kwamba alimpata kama mmoja kutoka mautini. Tumbo la uzazi la Sara lilikuwa limekufa, na Ibrahimu alikuwa mgumba, kwa hivyo hapakuwa na njia. Na yule mvulana. . .Ibrahimu alikuwa na umri wa miaka mia, Sara alikuwa na tisini, kwa hivyo mwana alikuja kwa Neno lililoahidiwa. Mungu yule yule aliyefanya ahadi, kasema, "Mimi nitakufanya wewe baba wa mataifa," baada ya miaka ishirini na mitano, na akiwa na umri wa miaka mia, yeye na mkewe walipata mtoto. Ikiwa Mungu alimwambia akamtoe sadaka, Mungu alikuwa na uwezo wa kumfufua. Amina.

187 Mungu asifiwe, ndugu zanguni. Najisikia vizuri. Najisikia kitawa. Kwa hivyo najisikia vyema jinsi gani! Mimi najua jambo hili moja, Yeye anaweza kumfufua tena. Tutasimama juu ya Neno lisilogoshiwa la Nuru ya wakati huu! Mungu atatufufua

kizazi hiki kitakapotokea, kama Taa zinazoangaza dhidi ya kizazi hiki. Amina.

188 Si ajabu Yeye alisema, “Malkia wa Kusini atasimama katika siku ya Hukumu, pamoja na kizazi chake, na kuhukumu hiki; kwa sababu alikuja toka pande za mwisho za dunia, ili asikie hekima ya Sulemani, na, tazama, hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani.” Jinsi gani yule maskini malkia mbali huko, kafiri, alivyoona Nuru hiyo, na kuja maili kadhaa kupitia jangwani, miezi mitatu mgongoni mwa ngamia, kusikia hekima ya Sulemani, na wao wakisimama papo hapo, huku Sulemani akiwa mfano, sura Yake.

189 Na basi wakaja na kuona Wesley, Luther, wengine wote, medhehebu nyuma huko, yakiwa umbo na mfano wa kile kinachotendeka sasa, na wao hutembea moja kwa moja kupitia Kwake. Loo! Sawa.

190 Kwa, kwa hivyo mwaka mpya unakusudiwa na Mungu, kukusudiwa tu kudumu katika Neno Lake. Tembea pale Neno linasema utembee tunapokuja sasa kumalizia, kama wale wengine, Mzao aliyeteuliwa walivyofanya katika siku yao walipokuwa Neno. Walifanya nini? Walitembea ndani Yake, ikiwa walikuwa Mbegu iliyoteuliwa katika nyakati zile zingine, kwa sababu Yeye ni Neno lisilokosea. Ni wangapi wanaamini ya kwamba Yesu Kristo ni Neno? [Kusanyiko la sema, “Amina “—Mh.] Loo, jamani!

191 Nilisikia kipindi hivi majuzi, cha dhehebu fulani la watu, Bwana H.M.S. Richards alisema alikuwa “ameisha andika kitabu cha mwaka.” Sitaki kubishana na mtu kama huyo. Ingawaje, akiwa wa dhehebu la sabato, mimi sikubaliani na fundisho la Wasabato, bali hakika nampenda huyo mtu. Bali sitakubaliana naye. Hicho kinaweza kuwa kitabu cha mwaka mpya cha H.M.S Richards.

192 Lakini Kitabu changu na Kitabu chako, kwa mwaka mpya, ni kile Kitabu cha mwaka wa zamani, Biblia, Neno la Mungu. Kifanye tu kiishie kile kilichoahidi kuishia. Naam, bwana. Na kila mwaka ujao, na kila mwaka ulioisha kuwepo, Yeye ni Mungu wa Milele anayeishi kupitia Neno la Milele ambalo Yeye alilinena, wakati kila Kweli ya Biblia na kila ahadi ndani Yake imeisha thibitishwa, kama imeishawahi kuwa katika miaka yote.

193 Jinsi Mungu alivyoahidi ya kwamba Yeye angaliangamiza ulimwengu kwa maji, na kuthibitisha hilo kwa Musa. . . au kwa Nuhu.

194 Yeye aliahidi ya kwamba angemtuma mkombozi, na kuwatoa Israeli Misri; walikuwa wameishakaa kwa miaka mia nne. Yeye alifanya hivyo hasa.

195 Naye aliapa ya kwamba yeye atamwinua Daudi; na jinsi Daudi angalikuwa mwa—mwana; Kristo angalikuwa mwanawe,

kupitia Daudi Kristo angetokea. Jinsi Yeye alivyoapa ya kwamba Yeye angetenda hilo; Yeye akatenda hilo tu.

196 Yeye aliahidi atamtuma Yohana Mbatizaji, kabla ya kuja kwa Yesu Kristo. Yeye alifanya hilo tu.

Yeye aliahidi atamtuma Masihi. Yeye alitende hilo tu.

197 Yeye aliahidi ulimwengu ungaliingia katika kundi kuu la madhehebu na kuunda utaratibu, nguvu, zijulikanazo kama yule mnyama, na atakuwa huko akiketi juu ya milima saba. Ikafanyika vivyo hivyo hasa.

198 Jinsi kanisa lingewatesa, hadi mauti. Wao walifanya vivyo hivyo hasa.

199 Jinsi wangalitoka wakati wa matengenezo! Wao walitenda vivyo hivyo hasa. Jinsi alivyoahidi itakuwa katika kila wakati!

200 Na Yeye aliahidi kwa ajili ya wakati huu. Na Yeye yuko hapa, leo, akilifanya Neno hilo liishi, sawasawa tu na vile alifanya hapo mwanzoni. Bila shaka.

201 Na kila ahadi itakapotimizwa, "mauti imemezwa kwa ushindi," Yesu atakuja. Na, wa mwisho akithibitishwa, ndipo kutakuja amani ya Milele duniani, na shalom ya Milele. Shalom ya Milele, amani, itadumu duniani.

202 Alipokuja Yesu, Mfalme wa Amani, kwa nini hakukuwako amani? Kwa sababu Neno lote halikutimizwa katika siku Yake. Yeye analitimiza leo. Lakini wakati Neno lote Lake lililoahidiwa, ambalo lilikuwa wazo la Mungu . . .

203 *Neno* ni "wazo likielezwa." Mungu katika kuwaza Kwake, aliliwazia, na kulinena kupitia manabii Wake, na sasa halina budi kutimizwa. Na, wakati, Yeye alitutabiria sisi mambo haya hivi kwamba hatutafanya kosa na kusitasita gizani hapo tunapoliona likitimizwa.

204 Sasa, Yeye aliahidi kumtuma Kristo mara ya Pili. Na kila mara afanyapo hivyo, Kristo ajapo mara ya Pili, kutakuwa na shalom ya Milele.

205 Sikizeni, marafiki, tunapomaliza. Kumbukeni, Biblia ndiyo chemichemi ya hekima yote. Haitokani na Daktari, Ph.D., L.L.D. Inatokana na Neno la Mungu.

206 Kulikuwa na Madaktari wa mambo ya Mungu wakiketi pale, kwa mamia, na Mvulana mdogo wa Miaka 12 akiwakemea, sababu Yeye alikuwa Neno. Yule Mvulana mdogo hakuwa na elimu yoyote, hata hivyo Yeye alikuwa Neno. Kwa sababu Yeye alikuwa Nuru iliyonenwa kwa siku hiyo, Yeye alikuwa akidhihirisha hilo Neno. Neno lilikuwa ndani Yake. Lilipaswa kuwa. Si ajabu kile Yeye alichosema kilitukia, kwa sababu alikuwa Neno. Mnaelewa? Wote wanaoelewa, semeni, "Amina." [Kusanyiko lasema, "Amina"—Mh.] Yeye alikuwa Neno.

207 Kumbukeni Biblia, si kitabu cha mwaka ambacho kimeandikwa na mtu. "Kila neno la mwanadamu liwe la uwongo, bali Langu Kweli."

208 Na madhehebu na dini, na—na kadhalika, yote yanarundikana mnapoingiza kundi la watu ndani Yake. Mungu kamwe hajashughulika na kundi kama hilo. Kama Yesu angekuja leo, Yeye angeungana na Wamethodisti; na Wabatisti, na Wasabato, Mashahidi wa Yehova; Christian Science, Wapentekoste, Wapresbateri? La, bwana. Hakika Yeye hangalijiunga nao.

209 Ni jambo la kibinafsi, wewe na Mungu. Hakuna watu wawili wanaokubaliana kabisa, walio sawa, hakuna vidole gumba viwili vilivyo sawa. Mungu hushughulika na mtu binafsi. Na unajuaje ikiwa amekosea au la? Basi tazama nyuma uone kama anaambatana na Neno. Ikiwa anaambatana na Neno, basi Mungu anamshughulikia; la sivyo, kitu kingine kinamshugulikia. Waona? Hiyo ni kweli.

210 Kumbukeni, Biblia, ni chemichemi ya hekima yote, na inashikilia ndani yake matumaini yote ya wakati ujao. Shalom, amani ya Mungu!

211 Kama hadithi ilivyosimuliwa wakati mmoja, juu ya mvulana mdogo aliyempoteza babaye kabla hajakua vya kutosha kumwona babaye; alikuwa tu kitoto kichanga alipokufa babaye. Siku moja alifikia umri wa miaka kumi, kumi na miwili. Alikuwa na ndugu mwingine aliyeitwa Yohana. Alimwendea nduguye, akasema, "A-haa, Yohana," aliyempita umri kwa miaka kadha, kasema, "una, unamkumbuka baba?"

Kasema, "Naam."

Kasema, "Alikuwa namna gani?"

212 Kasema, "Vema, yeye alikuwa mtu mrefu, naye alikuwa mtu mzuri sana. Alikuwa mwema kwa mama daima, na alikuwa mwenye huruma kwa—kwangu, na mwenye fadhili kwa kila mtu."

Yeye akasema, "Vema hayo ndiyo yote ujuayo juu yake, Yohana?"

213 Akasema, "Vema, nitakuambia." Kasema, "Henry," kasema, "kila mtu husema ya kwamba mimi—mimi ninafanana naye." Kisha akasema, "Kila mtu husema ya kwamba mimi nina tabia kama yake."

214 Yeye akasema, "Loo, hilo ni njema! Hilo ndilo nitakalo kujua." Kasema, "Nikuonapo wewe, namuona baba yangu."

215 Ndiyo hiyo. Wakati u—ulimwengu unapomwona Yesu Kristo, itakuwa ni ndani yako," wakati hili Neno ambalo limeandikwa kwa ajili ya leo.

216 Unamwona Yesu wapi katika Daudi? Wakati Neno lilipodhihirishwa kupitia kwake.

217 Unamwonaje Kristo, Mungu katika Eliya, katika lile gari likienda Mbinguni, wamwona Yesu katika Eliya? Kwa sababu, Neno lilithibitishwa.

218 Ulilionaje katika Musa? Yesu alikuwa ndani ya Musa. Biblia ilisema hivyo. Waona, hiyo ni kweli, Yeye alikuwa kijiti kilichowaka moto kilichokuwa pamoja na Musa jangwani.

219 Watu watamjuaje Yesu Kristo? Wakati wao, yeye, amwonapo ndani yako, wanapomwona Yesu ndani yako. Kwa kuwa, Yeye alisema, "Kazi nizifanyazo Mimi nanyi mtazifanya pia. Kubwa kuliko hizi mtazifanya kwa sababu naenda kwa Baba." Hiyo ni kweli? [Kusanyiko, "Amina."—Mh.] Hivyo ndivyo wao, ulimwengu ujuavyo.

220 Si kwa sababu Wapentekoste wa Umoja ni wakubwa kuliko Wapentekoste wa Upili, au wa Upili ni wakubwa kuliko wa Utatu, au chochote mlicho nacho; si kwa sababu Wamethodisti ni wakubwa kuliko Wabatisti; au Wabatisti wa Kusini wakipokea tuzo mwaka huu la—la makanisa yote ya Wabatisti, Waprotestanti wote. Wao wana washiriki wengi zaidi mwaka huu, kuliko yo yote ya yale mengine, nasikia, kulingana na hesabu. Hiyo haiwafanyi wao kuwa na tofauti yoyote. Mungu hawajui kwa hesabu yenu. Makafiri wanawashinda kwa wingi, wakati wowote. Wakatoliki wamewapata ninyi nyote. Uisilamu umewapata wote. Mwaona?

221 Unajulikana Yesu Kristo anapoishi ndani yako, kwa Uhai Wake, na Neno lililoahidiwa kwa ajili ya siku hii linapojionyesha lenyewe. Unaona?

222 Sasa Neno lile lile lililoonyeshwa katika Musa halingeweza kuonyeshwa katika Eliya, kwa sababu hiyo ilikuwa siku nyingine. Lile lile lililoonyeshwa katika Nuhu halingalikuwa katika Musa, kwa sababu, waona, Nuhu alijenga safina, Musa aliwaongoza watu, sawa tu na kile kilichoahidiwa. Nuru ile ile iliyoonyeshwa katika mmoja, haikuwa katika yule mwingine, bali mmoja aliambiana ya yule mwingine.

223 Agano Jipya lote hunena juu ya wakati huu. Yesu Kristo hunena juu ya wakati huu. Ni nani, basi, mtu fulani? Ni Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, akidhihirisha, akionyesha Nuru juu ya Neno ambalo Yeye aliahidi kwa ajili ya siku hii. [Ndugu Branham anagonga mara mbili juu ya mimbari—Mh.]

224 Mtu akuonapo ukiishi kama Yeye, aonapo tabia yako na mwenendo wako na Neno likiwa sawa tu kama Yeye alivyokuwa, Neno likidhihirishwa, basi watu watamwona Yesu Kristo. Hawatapaswa kutazama mahali pengine, kusema, "Kanuni *hii* ya imani hufundisha nini, kanuni *ile* ya imani hufundisha nini?" Watajua kile alicho Mungu wakuonapo wewe.

225 Shalom, amani ya Mungu na iwe Nuru juu yenu! Na Neno la Mungu linapothibitishwa katika wakati huu, kabisa, na ulione na kuliamini, shalom kwako!

226 Kabiliana na mwaka mpya na hili, mweke Yeye kama Daudi alivyosema, "Nitamweka Yeye mbele zangu daima. Kwa sababu Yeye yuko mkono wangu wa kulia, sitatikisika." Ikiwa utakutana na mauti mwaka huu, ina tofauti gani? Mungu aliahidi atakufufua. Ikiwa ajali itakuua, ina tofauti gani? Una Uzima wa Milele, "Nitamfufua katika siku za mwisho." Amina. Vipi ikiwa chochote kitatendeka? Haidhuru ni kitu gani, hakuna kitu kinachoweza kututenganisha na upendo wa Mungu, ulio katika Kristo. "Njaa, hatari, uchi, haidhuru ni nini, hakuna kitu kinachoweza kututenganisha na upendo wa Mungu, ulio katika Kristo." Na Yeye ni Neno. Shalom!

227 Hebu na tuinamishe vichwa vyetu. Sasa kila mtu inamisha kichwa chako punde tu. Amani ya Mungu!

228 "Kuu . . ." [Mahali patupu kandani—Mh.] "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, walipokuwa wakila, wakinywa, wakioa, wakiolewa," Reno, Nevada, na ulimwengu wote wa taa nyekundu, "ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwa Mwana wa Adamu."

229 "Kama ilivyokuwa katika Sodoma," ambapo Mungu alidhihirishwa katika Binadamu ambaye Ibrahimu alimwita Elohim, Yule ajitoshelezaye, akisimama pale, akala nyama, akanywa maziwa, na mkate, na angeweza kusema kile Sara alichokuwa akiwazia nyuma yake, nyuma Yake, katika hema. Yeye alisema, "Hiyo itarudi tena katika kuja kwa Mwana wa Adamu." "Kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona Mimi tena; bali ninyi mtaniona, kwa sababu nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari."

230 Wayahudi wanarudi nchini mwao. Mambo ambayo yanatendeka, yaliyo katika siku hii, yangenizuia kuwambieni nusu ya yale yanayotendeka, lakini tunayaona. Ni nini? Neno likidhihirishwa.

231 Mnafikiria Waebrania walifanya nini walipoona Neno likidhihirishwa, kwa ahadi? Walijitayarisha kuondoka nchini.

232 Kama hauko tayari leo, rafiki, anza mara moja mwaka huu mpya, uanze huku mkono wako umo katika mkono wa Mungu, Neno la Mungu moyoni mwako, ukisema, "Bwana Yesu, sijui ni sehemu gani ya hii Taarabu ambayo Wewe unataka nicheze, bali kijapo kile kiungo kwangu kuteswa, kuchekelewa, kudhihakiwa, ningali najitahidi kusimama kusudi Taarabu Yako isije ikachafuliwa kwa ajili yangu. Nitadumu sawa na Neno Lako, haidhuru liwe ni nini. Nitadumu papo hapo. Na mauti yabishapo hodi mlangoni mwangu, hiyo ni sehemu ya Taarabu. Hapo nitajua, ya kwamba, bila shaka kama tu vile mauti yatapiga hodi mlangoni mwangu, ufufuo pia utapiga hodi

mojawapo ya siku hizi, na Wewe utaniinua tena.Ni sehemu ya Taarabu Yako. Bwana, nijalie niwe sehemu leo, sivyo?"

233 Ni wangapi wangalitaka kuweka nadhiri hiyo, na kusema, "Kuanzia mwaka huu mpya, Ndugu Branham, kuanzia mkutano huu, sasa hivi, sasa namwahidia Mungu, kuchukua msimamo wangu, kutokushindwa kamwe kudumu sawa na Neno Lake lililoahidiwa, na kuishi sawasawa tu na vile Yeye alivyoliahidi, kwa upole na unyenyekevu; ili Mungu akayatwae maisha yangu na kuyaweka katika Taarabu Yake kuu, kundi lilo hilo Yeye atakalofufua katika siku za mwisho. Nitainua mkono wangu, Ndugu Branham, sio kwako, bali kwa Mungu. Nikumbuke katika maombi"? Mungu awabariki, kila mahali. Bwana awabariki. Mikono yangu iko juu, pia.

234 Bwana, nitwae mimi. Bwana Mungu, usiniache kamwe niiweke nia yangu, kama Yuda, juu ya dola moja zaidi, juu ya mtindo fulani wa ulimwengu, au mtu fulani akupapase mgongoni, na kusema, "Loo, Ndugu Branham, hili ni . . ." La, la. Mungu, usiliachilie hilo linipate. Nitashika njia pamoja na wachache wa Bwana wanaodharauliwa. Nitakuwa ndugu kwa mwanadamu, nifanye chochote niwezacho, Bwana, niwapende watu kwa moyo wangu wote. Lakini, Bwana, usiniache niondoke kwenye hili Neno. Ninataka kufufuka katika siku ya mwisho. Na ni wale tu ambao wamewekwa katika hii Taarabu kuu, Bwana, kama nilivyojaribu kuieleza adhuhuri hii, hao ndio watakaotokea mwishoni mwa—mwa ukurasa wa muziki, wakati ule ufufuo mkuu, na Malaika wote watapiga makofi na watakatifu wapige hatua wakiingia ndani. Ni hao ambao wameisha cheza hiyo sehemu katika mchezo huu mkuu wa kuigiza tunaocheza, naomba Bwana.

235 Tunajua ya kwamba katika mchezo wa kuigiza wanabadilisha vinyago, wanatoka kwenye jambo moja hata kwa lingine, na hivyo ndivyo wewe ulifanya. Ulitoka kwa Roho, Mungu, Yehova Mkuu, na kuvaa kinyago cha mwanadamu, ukabadilisha m—m—mfano Wako; Wewe ulibadilisha. Wewe Ulipiga hema Yako. Ulishuka kutoka kwa Mungu, na ukawa mwanadamu, upate kufa kumkomboa mwanadamu. Ulibadilisha kinyago Chako.

236 Basi Wewe umekibadilisha tena, na Wewe umejivisha kinyago ndani ya watu ambao wataamini na kutenda kulingana na Neno ambalo Wewe umekwisha andika hapa. Heri macho yale yalionayo, heri mioyo inayolipokea, heri masikio yanayolisikia kwa sababu kutatokea ufufuo Taarabu itakapokwisha. Mungu, hebu sisi sote tuwe pale, utafanya hivyo? Bariki kundi hili dogo.

237 Tukinena jinsi hii, Baba, tunajua ya kwamba kanda hii itaenda kote ulimwenguni. Na hapa kuna kikundi kidogo chema, kinachoketi hapa leo, wasikizaji hawa wanaoonekana hapa Phoenix. Ee Mungu, miaka kumi na mitano ya kuhubiri kugumu

na kukaripia pia, Mungu, Wewe unajua sababu yake, upendo! Upendo ni—ni kurudiwa. Upendo ni—ni kukemewa. Upendo ni kuadibisha.

238 Ee Mungu, hebu nikaungane pamoja na watu hawa juma hili, na Wewe upate kutuadabisha sisi, Bwana, kwa Neno Lako. Na tuone nguvu Zako zikiwainua wagonjwa na wanaoteseka, macho ya vipofu yakafunguliwe, Roho Mtakatifu aliye mkuu akaonekane dhahiri humu chumbani. Na kila mhudumu na kila kanisa lipate kuwaka moto. Na mkutano ujao wa wafanyi biashara, Bwana, upate kuufanya kila moyo wa wafanyi biashara, katika mji huu, kuwaka moto kwa ajili ya Mungu. Tujalie, Bwana. Hatujui la kufanya juu yake, zaidi ya kuomba na kuamini ya kwamba itatendwa. Twajikabithi sisi wenyewe Kwako, katika Yesu Kristo, Bwana wetu.

Na sasa hebu tusimame kwa miguu yetu.

239 Mimi ni hafifu wa usemi, hutamka maneno yangu vibaya, na nataka kusema hili kwa sababu nilijisikia nikishurutishwa kufanya hivyo. Ni wangapi walio hapa watainua mikono yao, ya kwamba mlielewa nilichomaanisha kwa "Taarabu ya Mungu"? Inua mkono wako. Ahsanteni. Vizuri. Mnaiamini? [Kusanyiko lasema, "Amina"—Mh.]

240 Basi, ni Taarabu, mwaona. Mtatambua ifikiapo kiungo, kila mtu anashangaa. Ninakiita kiungo. Sijui muziki; mwana-muziki aliye hapa, kwani, angem—angenisamehe kwa sababu ya njia yangu ya kishenzi. Lakini ni, wanapiga-piga hapa nje na wana kitu cha kucheza. Inaendelea pole pole sana, chini sana, unashangaa ni kitu gani; lakini, waona, ukiingia kwenye mdundo Wake, unaifahamu. Hiyo ndiyo njia pekee utakayomfahamu Mungu, ni kuingia katika mdundo Wake.

241 "Ni nini? Nitafanya nini? Ndugu Branham, mimi niko tu kama Mmethodisti, Mbatisti, au Mpentekoste wa kweli." Huo sio mdundo.

242 Mdundo ni Mungu. Mungu ni Neno. Neno ni Mungu. Mdundo wa Mungu, ni, kutii Neno Lake. Basi unapolitii Neno, Yeye huupiga mdundo huo ndani yako, ndiposa unachukua mahali pako. Kila ushukapo chini, chini, juu, chochote kile, wewe anajua vile viungo.

Wakati mwingine unasema, "Loo, huzuni za moyoni na majaribio!"

243 Si Mungu alisema "Katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema, ninapopiga Taarabu Yangu?" Na utaona ya kuwa basi umeteseka, na kuugua, na kudhulumiwa, kufanyiwa mzaha. Kumbaka, hiyo ni sehemu ambayo huenda namna hiyo. Kama hiyo sivyo ilivyo, basi Taarabu haina ulinganifu wa sauti.

244 Mtungaji mkuu anajua kilicho ndani yake hasa. Yeye anajua. Yeye alikujua wewe tangu mwanzo. Yeye aliliandika jina lako katika Kitabu cha Uzima Cha Mwana-Kondoo, kabla kuwekwa misingi ya ulimwengu. Unaamini hilo?[Kusanyiko lasema, "Amina."—Mh.] Yeye anajua unachopaswa kutenda. Haidhuru kinaenda chini jinsi gani, na jinsi inavyoonekana giza, haina budi kuwa hivyo.

245 Lakini, kumbukeni, kama ikididimia hata kwenye vivuli vya mauti, "Mimi ndimi ufufuo na Uzima; Mimi nitamfufua tena." Na ajapo huyo Kiongozi mkuu na kuweka fimbo chini, basi, "hapatakuwa na wakati baada ya hayo." Wakati yule Malaika, wa Ufunuo sura ya 10, atakapoweka mguu mmoja juu ya nchi na mmoja juu ya bahari, na upinde wa mvua juu ya kichwa Chake, Yeye aliapa, "hapatakuwa na wakati baada ya haya." Wakati huo ujapo, utafufuka katika wafu. Wakati wengine wao wanalala pale, wewe utaingia ndani.

246 Dumu katika Taarabu. Dumu katika Neno la Mungu. Haidhuru ni gumu jinsi gani, dumu pamoja Nalo, popote Mungu anapopiga.

247 Wakati mwingine Yeye husababisha shida kukata zile nyuzi, kukuweka huru. Yeye hufanya hivyo. Unasema, "Vema, sijui nifanyeje." Yeye anajua. Tofauti gani? Wewe una—unacheza tu ile sehemu. Yeye Ndiye anayekushika mkononi Mwake. Yeye hukuongoza.

248 Kumbukeni, yote hufanywa kwa ishara. Tunaona wakati tunamoishi, kwa ishara tunayoishi kwake, kwa hivyo tunajua kile Taarabu ifanyacho leo. Ni wakati wa kutengana, kuondosha Nuru gizani.

249 Hebu na tuiseme pamoja, msije mkasahau, kwa sababu najisikia kusema hili. [Ndugu Branham na kusanyiko wanasema pamoja—Mh.] "Ni kuiondosha Nuru gizani." Hebu tulisema tena. "Ni kuiondosha Nuru gizani."

250 Hiyo ndiyo Taarabu ya Mungu. Yeye anaionyesha mbinguni. Yeye alionyesha juu ya bao za kuandikia. Yeye alionyesha Kwake Mwenyewe. Aliahidi katika Neno. Tunaiona ikithibitishwa. Yeye anaitenganisha ngano na makapi. Yeye anaiondosha Nuru gizani.

251 Unamwamini Yeye, kwa moyo wako wote? [Kusanyiko lasema, "Amina."—Mh.] Hebu na tuimbe wimbo wetu mzuri, basi.

252 Na ninataka kusema neno kwa wachungaji, kwa dakika moja tu. Ndugu zanguni, Bwana awabariki. Ahsanteni kwa kuwaachilia makusanyiko yenu na kuwaleta hapa. Kwenu wachungaji huko nje, bila shaka nawashukuru. Niko hapa tu . . .

253 Hebu niseme, ndugu zanguni, huenda pakawa Wamethodisti, Wabatisti, Wapresbateria. Mnasikia, mimi hunena sawasawa

kwa Wapentekoste kama nilivyofanya kwenu? Sawasawa tu, mwaona. Sio . . .

254 Ikiwa siwezi kutokubaliana na mtu, vikali, na hata hivyo nimpende . . . Kwa sababu, kama sikubaliani naye, niwe tu sikubaliani, mimi mnafiki, sistahili kusimama hapa. Lakini ikiwa nilipingana naye kwa sababu ya ushirika na upendo na ufahamu, haidhuru anafanya nini, yeye yungali ndugu yangu wa thamani. Nasimama pamoja naye. Naam, bila shaka. Hiyo ni kweli hasa. Kama haimo moyoni mwangu, basi Mungu aniondoe kwenye mimbari hii, sistahili kuwa hapa. Hiyo ni kweli. Nasema hivyo kwa sababu ya upendo, na kitu ambacho ninakiona kikija. Na Yeye hajaniachilia nikosee juu yake, hata sasa, kwa sababu limekuwa Neno Lake daima. Kwa hiyo Mungu awabariki.

255 Sasa hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda mchache tu, na tuimbe wimbo huu mzuri, wa kale, ambao kwa kawaida sisi huuimba, "Nampenda, nampenda." Ikiwa mwenye kucheza kinanda, au yeyote yule, au walio na muziki, watatupa sauti yake kidogo, nakisia. Naam, sawa, hebu tuone kama tunaweza kuuimba basi bila muziki. Kila mtu pamoja sasa, vichwa vyetu vikiinamishwa.

Ninamenda, ninampenda
Kwa humpenda kwanza
Kaninunulia wakofu
Kalvari.

256 Nafikiri wamesimamisha kanda sasa. Mnaona, kanda hii huenda kila . . .

*Shalom* SWA64-0119
(Shalom)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili jioni, Januari 19, 1964, katika Ramada Inn kule Phoenix, Arizona, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2015 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org